# MUONGOZO WA MWALIMU WA KUMFUNDISHA MWANAFUNZI MWENYE UZIWIKUTOONA KATIKA ELIMU YA AWALI NA MSINGI DARASA LA I-II

# Utangulizi

## Usuli

Hali ya ufundishaji katika vitengo vya wanafunzi wenye uziwikutoona katika shule maalumu na shule jumuishi za msingi imekuwa na changamoto kutokana na kukosekana kwa mwongozo wa mwalimu wa kumfundishia mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona TET, imeandaaa Mwongozo wa Kufundishia Mwanafunzi mwenye Uziwikutoona katika Elimu ya Awali na Msingi Darasa la I na II. Aidha, mwongozo huu, umeandaliwa ili kumjengea mwalimu uwezo wa kujiandaa kikamilifu ili aweze kumwezesha mwanafunzi wenye uziwikutoona kujenga umahiri uliokusudiwa katika ufundishaji na ujifunzaji ndani na nje ya darasa.

Mwalimu unasisitizwa kuelewa aina ya wanafunzi wenye uziwikutoona ulionao darasani, ili kuandaa mpango binafsi wa kielimu wa mwanafunzi kulingana na mahitaji ya kipekee ya mwanafunzi husika. Pia, mwalimu unashauriwa kutumia zana/vifaa vya kufundishia kulingana na aina, uwezo na viwango vya ulemavu vya mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Pia, mwalimu unasisitizwa kutumia makunzi yanayopatikana katika mazingira yako katika kufaragua zana kulingana na mahitaji maalumu ya ujifunzaji wa mwanafunzi. Ufundishaji na ujifunzaji utafanikiwa endapo mwalimu utatumia kila matendo anayoyafanya mwanafunzi mwenye uziwikutoona kama fursa ya ujifunzaji na ufundishaji wake. Aidha, namna ya uwezeshaji wa umahiri umefafanuliwa katika kila hatua za kufuata katika ufundishaji na ujifunzaji ili kujenga umahiri uliokusudiwa kujengwa kwa mwanafunzi.

Jifunze zaidi kupitia Maktaba Mtandao

## Dhana ya Uziwikutokuona

Uziwikutoona ni hali ya mtu kuwa na changamoto ya kutosikia na kutoona kwa pamoja. Mtu mwenye changamoto hizi huitwa kiziwiasiyeona. Hali hizi zimegawanyika katika aina tano ambazo ni uziwikutoona kabisa, uziwi na uoni hafifu, uziwi hafifu na kutoona kabisa, uziwikutoona wastani, na uziwikutoona wenye ulemavu mwingine. Viwango vya changamoto za uoni na usikivu hutofautiana kati ya mwanafunzi kiziwiasiyeona mmoja na mwingine. Uziwikutoona unaweza kuambatana na changamoto nyingine kama vile; ulemavu wa akili, usonji na changamoto za matamshi. Hali hii husababisha mkwamo katika mfumo wa mawasiliano, ujenzi wa dhana maono na dhana sikizi, uhusiano katika jamii na ujongeaji. Hivyo, Kiziwiasiyeona asiye na changamoto za ulemavu mwingine kwa kawaida huwa hana tatizo katika ubongo wake zaidi ya kuwa na changamoto katika mawasiliano na ujongeaji kutokana na ulemavu alionao. Ni vyema kufahamu kuwa, hali ya uziwikutoona inategemea kiwango cha athari za usikivu na uoni kwa mtu. Ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona unahitaji mbinu na mikakati maalumu kutokana na kuwa kila mmoja ana changamoto za kipekee zisizofanana na mwingine hata wakiwa katika kundi moja la kiwango cha ulemavu. Hivyo, tofauti za wanafunzi wenye uziwikutoona husababisha changamoto za ufundishajia ujifunzaji kupitia mfumo wa kawaida wa elimu. Hata hivyo, wanafunzi wenye uziwikutoona wenye baki ya milango ya fahamu ya ujifunzaji ambao watamudu kujifunza kwa kujitegemea na kupata uzoefu wa kutosha, wanaweza kujumuishwa kwenye madarasa jumuishi na kupatiwa afua stahiki.

## Aina za uziwikutoona

Uziwikutoona umegawanyika katika aina tano ambazo ni:

a) Uziwikutoona kabisa: Ni hali ya kutosikia kabisa na kutoona kabisa
b) Uziwi na uoni hafifu: Ni hali ya kutosikia kabisa na uoni hafifu
c) Baki ya usikivu na kutoona kabisa: Ni hali ya kusikia kidogo na kutoona kabisa
d) Uziwikutoona wastani: Ni hali ya kusikia wastani na kuona wastani
e) Uziwikutoona wenye ulemavu mwingine: Ni hali ya milango ya fahamu ya uoni na usikivu kushindwa kufanya kazi inapochangamana na ulemavu mwingine.

## Historia ya elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona nchini Tanzania

Elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona nchini Tanzania ilianza mwaka 1993 katika kitengo cha elimu maalumu cha Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko iliyoko Jiji la Dar es

Salaam. Kitengo hiki kilianza kwa kuandikisha wanafunzi wawili, mvulana mmoja na msichana mmoja. Darasa la kwanza la wanafunzi hawa wawili wenye uziwikutoona lilianzia katika ofisi ya mwalimu. Mwalimu Medrine Gambo na Anjelika Mtwale ndiyo waliokuwa walimu wa kwanza wa wanafunzi hao. Mnamo mwaka 1994, wanafunzi wawili wenye uziwikutoona wavulana waliongezeka na ndipo darasa rasmi lilifunguliwa kwa ufadhili wa shirika lisilo la kiserikali la "Solidarity Human Rights Inclusion and Accessibility (SHIA)" kwa kushirikiana na Serikali chini ya Wizara ya Elimu.

Serikali kwa kushirikiana na mashirika ya SHIA na "Christoffel-Blindenmission (CBM)" walianzisha vitengo viwili (2) mwaka 2005 katika Shule ya Msingi Iringa Viziwi na Shule ya Msingi Mugeza - Viziwi. Uanzishwaji wa vitengo hivyo ulikwenda sambamba na mpango wa kuwaandaa walimu kwa njia ya semina za mafunzo kazini ili waweze kumudu ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye uziwikutoona kwa ushirikiano na shirika la "Perkins International" la Marekani.

Mwaka 2006, shirika la "Sense International Tanzania (SITZ)" lilipokea kutoka kwa SHIA na kuendelea kushirikiana na serikali katika kuboresha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona. Shirika hili kwa kushirikiana na TET lilianza mchakato wa kupata mwongozo kwa ajili ya wanafunzi wenye uziwikutoona. Aidha, mwaka 2010 TET kwa kushirikiana na SITZ walifanya utafiti kubaini uhitaji wa mwongozo huo kwa ajili ya wanafunzi wenye uziwikutoona.

Sambamba na utafiti huo, shirika la SITZ liliendelea kushirikiana na Serikali katika kuongeza vitengo hivyo hadi kufikia kumi (10) mwaka 2013. Vitengo hivyo ni Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko (Dar es Salaam), Shule ya Msingi Mugeza Viziwi (Bukoba), Shule ya Msingi Viziwi (Iringa), Shule ya Msingi Mwanga Viziwi (Kilimanjaro), Shule ya Msingi Buguruni Viziwi (Dar es Salaam), Shule ya Msingi Masasi Mchanganyiko (Lindi), Shule ya Msingi Msandaka Viziwi (Kilimanjaro), Shule ya Msingi Dongobesh Viziwi (Manyara), Shule ya Msingi Njombe Viziwi (Njombe) na Shule ya Msingi Tumaini Viziwi (Singida).

Matokeo ya utafiti yalionesha kuwapo na uhitaji wa mwongozo wa mwalimu wa kumfundishia mwanafunzi mwenye uziwikutoona kwani kila kitengo kilionekana kufundisha maudhui ya aina tofauti kulingana na uwezo na ujuzi wa mwalimu. Hivyo, TET imeandaa mwongozo huu kwa ufadhili wa SITZ.

Pia, shirika la SITZ limekuwa likishirikiana na shirika la "Perkins International" katika kuwajengea walimu na walimu mwega uwezo na ujuzi wa utoaji huduma ya elimu kwa wanafunzi wenye uziwikutoona.

## Lengo la mwongozo

Lengo la mwongozo huu ni kumwezesha mwalimu kumudu stadi za kumfundisha mwanafunzi mwenye uziwikutoona Elimu ya awali na Msingi Darasa na la I na II. Baada ya kufundishwa mwanafunzi anatarajiwa kupata maarifa, ujuzi na stadi za kujitegemea.

## Walengwa wa mwongozo

Mwongozo huu umeandaliwa kwa ajili ya walimu wanaowafundisha wanafunzi wenye uziwikutoona katika Elimu ya Awali na Msingi Darasa la I na II. Aidha, mwongozo huu unaweza kutumiwa na wadau wengine wa elimu kama vile; wakufunzi wa vyuo vya ualimu elimu maalumu, wathibiti ubora wa shule na vyuo, maofisa elimu, walimu mwega, wakuu wa shule, walimu wa wanaofundisha madarasa jumuishi, wazazi, walezi na watafiti.

## Umuhimu wa mwongozo

Mwongozo huu utasaidia kuboresha na kuimarisha njia na mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Aidha, mwongozo huu utamsaidia mwalimu kubaini hatua za kufuata wakati wa kumfundisha mwanafunzi ili kutekeleza shughuli zilizoanishwa katika mwongozo huu na katika vitabu vya kiada. Vilevile, mwongozo umeainisha baadhi ya mifano ya hatua za ufundishaji kwa baadhi ya umahiri ambayo unaweza kuitumia katika kumfundisha mwanafunzi mwenye uziwikutoona.

## Muundo wa mwongozo

Mwongozo huu umegawanyika katika sura nane ambazo ambazo ni; sura ya awali, kusoma, kuandika, demosntrate mastery of basic English language, kuhesabu, kuthamini utamaduni, sanaa na michezo, na kutunza mazingira, ambazo zimeundwa kwa kufuata umahiri mkuu. Umahiri mkuu mmoja umegawanyika katika umahiri mahususi, shughuli za kutendwa na majadiliano ya mwanafunzi kwa kutumia mbinu ya Tafakari, Husisha, na Tumia (THT).

## Matumizi ya mwongozo

Mwongozo utatumika sambamba na Mihtasari ya Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi Darasa la I na II. Kabla ya kutumia mwongozo huu mtumiaji anapaswa kurejelea taarifa zilizopo kwenye viambatisho ili zimsaidie katika:

a) Kufanya uchunguzi kwa mwanafunzi ili kuweza kubaini utendaji wa milango ya fahamu katika ujifunzaji wake.

b) Kuandaa mpango binafsi wa kielimu wa mwanafunzi.
c) Kuandaa jinsi ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango binafsi wa kielimu.
d) Kujaza fomu ya maendeleo.

Mwalimu unashauriwa kuzingatia kiwango cha uelewa wa mwanafunzi kwa kufanya uchunguzi/upimaji kwa kuzingatia maeneo yanayohitaji uchunguzi wadau wanaohitajika ili kuandaa mpango binafsi wa ujifunzaji. Mapendekezo ya maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma yazingatiwe ili mwanafunzi awekwe katika ngazi anayostahili kimasomo na kiutendaji.

## Uchopekaji wa masuala mtambuka

Masuala mtambuka yanayopaswa kuzingatiwa katika mwongozo huu. Mwalimu kumbuka kuzingatia uchopekaji wa masuala mtambuka wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Masuala haya ni kama; mazingira, elimu jumuishi, elimu ya jinsia, elimu ya amani, maadili, haki na wajibu wa mtoto, haki za binadamu, ulinzi na usalama, usalama barabarani, elimu ya fedha, elimu dhidi ya rushwa, ushirika na masuala ya muungano. Mwalimu unapaswa kuchopeka masuala mtambuka kwenye masomo bebezi wakati wa vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uhusiano wa suala mtambuka na umahiri husika.

# Sura ya Awali

## Utumiaji wa stadi za kujimudu

### Utangulizi

Sura hii inahusu namna ya kumjengea mwanafunzi mwenye uziwikutoona umahiri wa stadi za kujimudu Darasa la Awali. Katika sura hii, mwanafunzi mwenye uziwikutoona atajenga umahiri katika kutumia mafunzo kabilishi katika mazingira yake, kutumia mbinu za ujongeaji, kumudu stadi za kujitegemea, kushiriki katika shughuli za kijamii na kujikinga na magonjwa mbalimbali.

### Kutumia mafunzo kabilishi katika mazingira yake

**Shughuli ya 1:** Kutofautisha uelekeo kwa kutumia sehemu za mwili wake Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kubaini mielekeo mbalimbali kwa kutumia sehemu za mwili wake katika mazingira yake kama vile; juu, chini, nyuma, mbele, kulia na kushoto ili kuweza kuyamudu mazingira yake.

**Vifaa/zana:** Kamba ya kuanikia nguo, tanki la maji, choo, jiko na dira.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kutaja pande kuu nne za dunia ambazo ni kaskazini, kusini, mashariki na magharibi;
ii) upande wa juu ambao ni kichwa cha mwanafunzi mwenye uziwikutoona na kuhusianisha na kaskazini;
iii) kuonesha upande wa chini ambao ni unyayoni mwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona na husianisha na kusini;
iv) kuonesha upande wa kulia ambao ni kulia kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona husianisha na mashariki;
v) kuonesha upande wa kushoto kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona na husianisha na magharibi; na
vi) kutumia sehemu za mwili wake kuonesha pande kuu nne za dunia.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Je, katika dira unyayoni panaitwa upande gani?

i. Je, katika dira kulia panaitwa upande gani?
ii. Je, katika dira kichwani panaitwa upande gani?
iii. Je, katika dira kushoto kunaitwa upande gani?

**Husisha**

i) Choo cha darasa kipo upande gani wa dira?
ii) Jiko la shule lipo upande gani wa dira?
iii) Kamba ya kuanikia nguo ipo upande gani wa dira?

**Tumia**

Tumia pande za dunia kubaini muelekeo wa vitu vilivyopo darasani.

**Shughuli ya 2:** Kubaini uelekeo katika mazingira

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona, kubaini uelekeo wa juu, chini, kulia na kushoto, mbele na nyuma.

**Vifaa/zana:** Dira, chati ya alama za barabarani, taa za rangi mbalimbali, nguo za kuakisi mwanga.

**Hatua za kufuata:**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kujua mielekeo tofautitofauti katika mazingira ya ndani na nje ya darasa;
ii) kuwa kichwani kwake ni upande wa juu;
iii) kuwa upande wa tumbo lake ni uelekeo wa mbele;
iv) kuwa upande wa mgongoni kwake ni uelekeo wa nyuma;
v) kwamba upande wa nyayo zake ni uelekeo wa chini;
vi) kwamba upande wa mkono wake wa kulia ni uelekeo wa kulia; na
vii) upande wa mkono wake wa kushoto ni mwelekeo wa kushoto.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Shika tumbo utaje ni upande gani wa uelekeo?
ii) Shika kichwa utaje ni upande gani wa uelekeo?

**Husisha**

i) Kati ya mkono wa kushoto na kulia upi unautumia kula chakula?
ii) Kichwa chako kipo juu au chini ya mwili wako?

**Tumia**

Onesha uelekeo wa nyuma, mbele, chini na juu kwa kutumia sehemu zako za mwili.

**Shughuli ya 3:** Kubaini alama za kudumu na zisizo za kudumu

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kubaini alama za kudumu na alama zisizo za kudumu katika mazingira ya ndani na nje ya darasa mfano, viti, meza, majengo, kengele, harufu, joto, baridi, miti na maua ili kuzitambulisha kwa mwanafunzi mwenye uziwikutoona kwa usalama na afya yake. Vifaa/zana: Fimbo nyeupe, fimbo ya kieletroni, kikamba, ndoo, viti, meza, mlango.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha maeneo makuu na muhimu ndani na nje ya darasa mfano, maktaba, jikoni, chooni, bwaloni, bwenini, uwanjani, bustanini na bombani;
ii) kuhakikisha unabaini vitu salama na hatarishi vilivyomo ndani na nje ya darasa;
iii) kwa kutumia fimbo nyeupe au fimbo ya kielektroni mwelekeze mwanafunzi matumizi ya fimbo nyeupe na fimbo ya kielektroni;
iv) kutambua vitu salama na hatarishi vilivyomo ndani na nje ya darasa;
v) kuyatambua maeneo mbalimbali ndani na nje ya darasa mfano jikoni, chooni, shimo la taka na uzio;
vi) kuhakikisha usalama wake wakati wote unapomwelekeza ndani na nje ya darasa;
vii) kutambua vitu alama na ishara zinazoweza na kukumbuka njia na mwelekeo mfano, harufu, sauti, kelele;
viii) kutumia mazingira ya ndani na nje ya darasa kwa kuzingatia alama za kudumu na zisizo za kudumu; na
ix) kutumia maeneo na vitu katika kutambua uelekeo (alikotoka, alipo na anakokwenda.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Je, katika safari yako umekutana na vikwazo gani?
ii) Je, unapenda kwenda chooni kwa kutumia fimbo au kusindikizwa na mwenzako?

**Husisha**

i) Sehemu gani nyingine umewahi kuelekezwa na mwalimu?
ii) Je, unapata ugumu gani kwenda sehemu ambayo hujapewa maelekezo?

**Tumia**

i) Unapenda kutumia fimbo au mtu mwongozaji?
ii) Ni wakati gani mwingine unatumia fimbo nyeupe au fimbo ya kielektroni?

**Kutumia mbinu za ujongeaji**

**Shughuli ya 1:** Kubaini mbinu mbalimbali za ujongeaji

Shughuli hii inalenga mwanafunzi mwenye uziwikutoona kuzimudu stadi za kujimudu kwa kuzibaini mbinu mbalimbali za ujongeaji kama vile mbinu ya binadamu mwongozaji, mbwa mwongozaji na kushika fimbo nyeupe na mbinu ya kushika fimbo ya kielektroni.

**Vifaa/zana:** Binadamu, mbwa, fimbo nyeupe, fimbo ya kielektroni.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuchunguza maeneo mbalimbali na muhimu ya ndani na nje ya darasa;
ii) kuchunguza vitu mbalimbali kwa kuzingatia vilivyomo katika mazingira ya ndani na nje ya darasa;
iii) katika kutumia kifaa saidizi mfano, fimbo nyeupe na fimbo ya kielektroni katika kujongea;
iv) kujikinga na hatari kwa kumwelekeza mbinu za usalama;
v) kutumia vitu vinavyoonesha njia, alama na ishara kwa ajili ya usalama;
vi) kwa kutumia msaada wa mtu mwenye uoni, mwelekeze namna salama ya kushika mkono wa mwongozaji; na
vii) mbinu anuwai wakati wa kutembea, mfano anapopaswa kushuka, kupanda, kusimama, kuongeza au kupunguza mwendo au kupita sehemu nyembamba.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Ulijisikiaje ulipokuwa unaongozwa na binadamu?

ii) Vitu gani vya hatari ulivibaini?

**Husisha**

i) Unapotembea unapenda kuongozwa na binadamu au fimbo nyeupe au fimbo ya kielektroni?
ii) Ni nani anayekuongoza unapokwenda bwenini?

**Tumia**

i) Kuna umuhimu gani kujua mahali unapoishi?
ii) Nini hukuongoza unapokwenda darasani?

**Shughuli ya 2:** Kutumia mbinu za ujongeaji

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kutumia mbinu za ujongeaji kama vile matumizi ya fimbo nyeupe, fimbo ya kielektroni, usaidizi wa mbwa na kuongozwa na binadamu anayeona ili kukabiliana na kuyamudu mazingira.

**Vifaa/zana:** Fimbo nyeupe, fimbo ya kielektroni, mbwa mwongozaji na mtu mwongozaji

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuchunguza maeneo makuu na muhimu ya ndani na nje ya darasa;
ii) kuchunguza vitu muhimu vilivyomo katika mazingira ya ndani na nje ya darasa;
iii) kutumia kifaa saidizi mfano fimbo nyeupe katika kujongea;
iv) kujikinga na hatari kwa kumwelekeza mbinu za usalama;
v) kutumia vitu vinavyoonesha njia, alama na ishara kwa ajili ya usalama;
vi) namna salama ya kushika mkono wa mwongozaji; na
vii) kuzijua mbinu anuwai wakati wa kutembea, mfano anapopaswa kushuka, kupanda, kusimama, kuongeza au kupunguza mwendo.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Ulijisikiaje uliposhikwa mkono?
ii) Vitu gani vya hatari ulivibaini?

**Husisha**

Kati ya mbwa na binadamu muongozaji unapenda kuongozwa na nini?

**Tumia**

i) Unapokwenda darasani hutumia fimbo nyeupe au binadamu mwongozaji
ii) Unaongozwa na nini unapokwenda bwenini au nyumbani?

**Shughuli ya 3:** Kutumia mbinu za kujilinda wakati wa kujongea katika mazingira aliyopo.

Shughuli hii inalenga kumwelekeza mwanafunzi mwenye uziwikutoona kujilinda wakati wa kutumia mbinu za ujongeaji. Usalama wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona ni muhimu sana, hivyo ni lazima afahamu kutumia mbinu za ujongeaji kwa hadhari kubwa kwa ajili ya usalama na afya yake.

**Vifaa/zana:** Fimbo nyeupe, mtu mwongozaji

**Hatua za kufuata**

i) Kwa kumtumia mtu mwongozaji, mwongoze mwanafunzi:
ii) kujikinga na hatari kwa kumwelekeza hatua za kufuata wakati wa kuongozwa na mtu anayeona;
iii) asimame umbali wa nusu hatua nyuma ya mwongozaji;kukunja mkono wake na kushika kiwiko cha mwongozaji sehemu ya chini;
iv) kutumia mkono wake ulio huru kulinda sehemu ya juu ya mwili wake hasa mnapopita sehemu finyu kama vile mlangoni;
v) mwelekeze mwanafunzi mwenye uziwikutoona, kukaa upande wako wa kulia wakati wote na kubadilisha pale inapohitajika; na
vi) wakati wote hasa mnapofika kwenye vikwazo kama vile ngazi, kona au barabara finyu kwa kusimama kidogo.

**Kwa kutumia fimbo nyeupe, mwongoze mwanafunzi:**

i) kujikinga na hatari kwa kumwelekeza hatua za kufuata wakati wa kutumia fimbo nyeupe;
ii) namna ya kushika fimbo nyeupe kwa mkono wake huku kidole gumba kikiwa kimenyooka sambabamba na fimbo nyeupe;
iii) namna ya kutembeza fimbo nyeupe kushoto na kulia ili kutengeneza nusu duara mbele yake ili kujihakikishia usalama; na
iv) kuweka mkono uliohuru juu au chini anapohisi kuna mazingira ya hatari kuzuia kuumia.

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Ulijisikiaje ulipotumia fimbo ya kielektroni kutembea?
ii) Vikwazo gani ulikutana navyo njiani ulipotembea kwa kutumia fimbo nyeupe?

**Husisha**

Je, unapenda kutembea kwa fimbo nyeupe au kushikwa mkono? Kwanini?

**Tumia**

Mkono wako ambao haushiki fimbo hufanya kazi gani wakati wa kutembea?

**Kumudu stadi za kujitegemea**

**Shughuli ya 1:** Kubaini sehemu za mwili wake

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona, kubaini sehemu za mwili kama vile juu, chini, mbele na nyuma pamoja na kazi zake ili kushiriki katika shughuli za kila siku.

**Vifaa/zana: Picha, chati**

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) andaa picha mguso inayoonesha sehemu za mwili wa binadamu, kinyago;
ii) kubaini sehemu za juu za mwili wa binadamu;
iii) kubaini sehemu za chini za mwili wa binadamu;
iv) kubaini sehemu za nyuma au mbele za mwili wa binadamu;
v) kuonesha sehemu za mbele au za nyuma za mwili wa binadamu kama vile kichwa, miguu, pua, macho, mikono na miguu; na
vi) kutaja kazi ya kila sehemu.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira

**Tafakari**

i) Je, una mikono mingapi?
ii) Je, unaweza kushika sehemu ya juu ya mwili wako?

**Husisha**

Miguu yako ipo sehemu gani ya mwili?

**Tumia**

Ni mkono gani unaotumia wakati wa kula?

**Shughuli ya 2:** Kubaini vifaa vya usafi wa mwili wake

Lengo la shughuli hii ni kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona, kubaini vifaa vya usafi wa mwili wake, kujua matumizi ya kila kifaa ili kuvitumia katika shughuli za usafi binafsi na usafi wa mazingira.

**Vifaa/zana:** Ndoo, beseni, sabuni, taulo, dodoki, mswaki, dawa ya meno, maji, fagio, dekio, jembe, reki, zolea, kitana na mafuta ya kupaka.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandaa vifaa vya usafi kulingana na shughuli inayohusika;
ii) kutambua vifaa vinakopatikana;
iii) kutambua kifaa kimojakimoja;
iv) kueleza matumizi ya kila kifaa kulingana na shughuli inayohusika;
v) kujua kanuni za matumizi ya kila kifaa kwa kuzingatia usalama;
vi) namna ya kukifanyia usafi kifaa baada ya kukitumia; na
vii) kutumia kanuni bora za utunzaji wa vifaa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Je ni vitu gani viwili unavitumia kwa usafi wa mwili wako?
ii) Unafanya usafi wa kinywa chako wakati gani?

**Husisha**

Ni vitu gani unapaswa kuviandaa kabla ya kwenda kuoga?

**Tumia**

i) Unatumia vitu gani wakati wa kuoga?
ii) Unatumia kitu gani kuchania nywele zako?

**Shughuli ya 3:** Kuonesha uwezo wa kufanya usafi wa mwili

Shughuli hii imelenga kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kujitegemea katika shughuli za usafi wa mwili kama vile; kupiga mswaki, kuoga na kuchana nywele.

**Vifaa/zana:** Ndoo, beseni, sabuni, taulo, dodoki, mswaki, dawa ya meno, maji, fagio, dekio.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandaa vifaa vya usafi vitakavyotumika katika shughuli ya usafi wa mwili;
ii) kubaini vifaa vitakavyotumika kwenye shughuli ya usafi wa mwili;
iii) kupitia na kutambua kifaa kimoja kimoja;
iv) kuonesha matumizi ya kila kifaa;
v) kuzingatia hatua za shughuli inayohusika;
vi) kupitia/ kuhakiki kazi kuanzia mwanzo hadi mwisho ili kujiridhisha;
vii) kusafisha kwa uangalifu vifaa vilivyotumika katika shughuli za usafi; na
viii) kutunza vifaa vya usafi wa mwili kwa kuweka katika mazingira salama.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Ni vitu gani hutumika kufanyia usafi wa mwili?
ii) Ni shughuli ipi ya usafi wa mwili unayoipenda?

**Husisha**

i) Ni shughuli gani ya usafi wa mwili uliyowahi kuifanya ukiwa nyumbani?
ii) Unaoga mara ngapi kwa siku?

**Tumia**

i) Mara baada ya kuamka unafanya nini?
ii) Ili meno yawe safi na salama unapaswa kufanya nini?

**Shughuli ya 4:** Kuonesha uwezo katika stadi za kujitegemea

Shughuli hii imelenga kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kumudu stadi za kujitegemea kama vile kula, kunywa, kuvaa na kutumia choo.

**Vifaa/zana:** Chakula, chai, nguo, choo

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubaini kikombe, maji, chai na choo;
ii) kushika kikombe cha maji au chai na kunywa;
iii) kumudu kuvua nguo au soksi alizovaa;
iv) kuvaa nguo au soksi;
v) kumudu kuvaa nguo na viatu;
vi) kutambua choo kilipo;
vii) kumudu jinsi ya kutumia choo; na
viii) aweze kufanya usafi wa mwili wake baada ya kujisaidia.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Ni vifaa gani unatumia kunywa maji?
ii) Ni nguo gani unayopendelea kuivaa?

**Husisha**

i) Ni nani anayekusaidia kuvaa nguo ukiwa bwenini au nyumbani?
ii) Ni chakula gani unachokula asubuhi?

**Tumia**

i) Unatumia kikombe kufanyia nini?
ii) Unapokula chakula unatumia nini?

**Kushiriki shughuli za kijamii**

**Shughuli ya 1:** Kubaini alama za taifa

Shughuli hii inalenga kumwandaa mwanafunzi mwenye uziwikutoona kuwa mzalendo kwa kuzibaini alama za Taifa la Tanzania kama vile; Wimbo wa Taifa, Mwenge wa Uhuru, Fedha, Ngao ya Taifa, Bendera ya Taifa na Sikukuu 3 za Kitaifa ambazo ni Uhuru wa Tanganyika, Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

**Vifaa/zana:** Chati iliyochorwa ngao ya taifa, bendera ya taifa, fedha na kalenda

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) andaa picha, picha mguso, vitu halisi, vifani na michoro au michoro mguso inayoonesha alama za taifa;
ii) kutambua vifaa vitakavyotumika;
iii) kutambua matumizi ya kila kifaa;
iv) kubaini kanuni zinazotumika katika kila alama; na
v) kubaini sababu za kuwapo kwa kanuni hizo.

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira

**Tafakari**

i) Sarafu ya shilingi mia moja ina alama gani?
ii) Bendera ya Taifa ina rangi ngapi?

**Husisha**

i) Kati ya rangi nyeusi na buluu katika bendera ya taifa unaipenda ipi?
ii) Ulishawahi kuona, kupapasa au kugusa, ngao ya taifa?

**Tumia**

i) Ni alama gani ya taifa ambayo huwezesha kununua na kulipia vitu?
ii) Alama gani ya taifa inawakilishwa na mwanamke na mwanamume?

**Shughuli ya 2:** Kufafanua alama za taifa

Shughuli hii inalenga kumwandaa mwanafunzi mwenye uziwikutoona kuwa mzalendo kwa kuziheshimu na kuzithamini alama za taifa kwa vitendo.

**Vifaa/zana:** Chati iliyochorwa ngao ya taifa, bendera ya taifa, mwenge wa uhuru, pesa na kalenda

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) andaa picha, picha mguso, vitu halisi, vifani na michoro inayoonesha alama za taifa;
ii) kubaini alama za taifa zitakazotumika;
iii) kubaini kila alama ya taifa;
iv) kufafanua umuhimu wa alama zinazotumika katika kila alama;
v) kuelewa sababu za kuwapo kwa kanuni hizo; na
vi) kutumia alama moja baada ya nyingine mfano kuimba wimbo wa taifa, kuchora bendera ya taifa, kwa kuzingatia kanuni.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Maeneo gani bendera ya taifa upeperushwa?
ii) Wimbo wa Taifa huimbwa ili kuashiria nini?
iii) Chora bendera ya taifa na uipake rangi.

**Husisha**

i) Rangi nyeusi katika bendera ya taifa inawakilisha nini?
ii) Unasimamaje unapoimba wimbo wa taifa?

**Tumia**

i) Bendera ya taifa inapandishwa na kushushwa wakati gani?
ii) Fedha zina kazi gani?

**Shughuli ya 3:** Kubaini muundo wa uongozi katika ngazi mbalimbali

Shughuli hii inalenga kumwandaa mwanafunzi mwenye uziwikutoona kuwa mzalendo kwa kubaini muundo wa uongozi kuanzia katika ngazi ya familia, shuleni, kijiji, kata, wilaya, mkoa na taifa ili kuheshimu sheria, kanuni na taratibu zilizopo katika jamii.

**Vifaa/zana:** Vipeperushi, matini mbalimbali, majarida, runinga, picha, picha mguso, manila, gundi, kalamu za risasi.

**Hatua za kufuata:**

i) shirikiana na wanafunzi wenye uziwikutoona, kuchora muundo wa uongozi katika ngazi za familia, shule, kijiji, kata. wilaya, mkoa na taifa;
ii) mwongoze mwanafunzi mwenye uziwikutoona, kubandika mchoro huo ukutani;
iii) mwongoze mwanafunzi mwenye uziwikutoona, kubaini muundo wa uongozi katika ngazi za familia, shule, kijiji, kata, wilaya, mkoa na taifa;
iv) mwongoze mwanafunzi mwenye uziwikutoona, kuelezea muundo wa uongozi katika ngazi ya familia, shule, kijiji/mtaa, kata, wilaya, mkoa na taifa;
v) andaa ziara ya mafunzo kwa wanafunzi wenye uziwikutoona, (ziara hiyo ifanyike katika mazingira halisi yanayofikika;
vi) mwongoze mwanafunzi mwenye uziwikutoona, kufanya ziara ya kimafunzo katika ofisi ya mwalimu mkuu, kata/kijiji ili kuona namna muundo wa uongozi unavyofanya kazi; na

vii) waulize maswali kutokana na ziara hiyo

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira

**Tafakari**

i) Nani ni kiongozi wa familia yenu?
ii) Nani ni kiongozi wa shule yenu?

**Husisha**

i) Kiongozi wa familia yenu anaitwa nani?
ii) Kiongozi wa shule yenu anaitwa nani?

**Tumia**

i) Je, wewe umeshawahi kuwa kiongozi?
ii) Kuna faida gani ya kuwa na kiongozi wa darasa?

**Shughuli ya 4:** Kubaini vitendo vya unyanyasaji na udhalilishaji

Shughuli hii inalenga kumwandaa mwanafunzi mwenye uziwikutoona, kubaini matendo ya unyanyasaji na udhalilishaji anayoweza kufanyiwa, mfano kuitwa majina yanayodhalilisha, kubaguliwa, kutomaswa, kubakwa na kulawitiwa.

**Vifaa/zana:** Chati inayoonesha orodha ya matendo ya unyanyasaji na udhalilishaji

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandaa orodha ya matendo yanayoonesha unyanyasaji na udhalilishaji;
ii) kubaini matendo yanayoonesha unyanyasaji na udhalilishaji katika jamii;
iii) kubaini sababu za uwapo wa matendo ya unyanyasaji na udhalilishaji katika jamii;
iv) kuelewa sababu za uwapo wa matendo ya unyanyasaji na udhalilishaji;
v) namna ya kujitenga na matendo ya unyanyasaji na udhalilishaji katika jamii; na
vi) namna ya kutoa taarifa kuhusu matendo ya unyanyasaji na udhalilishaji kwa mwalimu, mzazi na katika vyombo vya usalama vilivyopo katika jamii yake.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Je, ulishawahi kuitwa jina linalokudhalilisha?

ii) Je, ulichukua hatua gani?

**Husisha**

i) Je, ndugu zako wanakutenga kwenye shughuli za kijamii?
ii) Nani ni rafiki yako shuleni?

**Tumia**

i) Tukio gani la udhalilishaji ambalo ulikwishawahi kulitolea taarifa shuleni au nyumbani?
ii) Nani anakunyanyasa shuleni au nyumbani?

**Kujikinga na magonjwa mbalimbali**

**Shughuli ya 1:** Kubaini aina za magonjwa

Sehemu hii inalenga kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona, kuyafahamu magonjwa mbalimbali yanayoweza kuathiri afya yake kama vile malaria, VVU na UKIMWI, kipindupindu, kuhara, kuhara damu, UVIKO 19 na kifua kikuu na dalili za magonjwa na namna ya kujikinga.

**Vifaa/zana:** Vitu vyenye ncha kali, picha, michoro, vipeperushi, video, miswaki, runinga.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

Kuandaa orodha ya majina ya aina za magonjwa mbalimbali yanayowaathiri binadamu;

i) kutaja aina ya ugonjwa aliowahi kuumwa;
ii) kutaja sababu za kuumwa ugonjwa huo;
iii) kutaja magonjwa mengine ambayo alishawahi kuugua;
iv) kutaja magonjwa ambayo watu wake wa karibu waliwahi kuugua;
v) kutaja sababu za wao kuugua magonjwa hayo; na
vi) kubaini magonjwa mengine ambayo ni hatarishi katika jamii.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Je, unadhani ni magonjwa gani yanaweza kukutenganisha na watu?
ii) Leo umejifunza kuhusu ugonjwa gani?

**Husisha**

Ulishawahi kuugua ugonjwa gani?

**Tumia**

i) Ukiumwa unapelekwa wapi?
ii) Unafanya nini ili kuimarisha afya yako?

**Shughuli ya 2:** Kufafanua dalili za magonjwa mbalimbali

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona, kujenga stadi za kujimudu kwa kuchambua dalili za magonjwa mbalimbali yanayopatikana katika jamii ili kubaini njia za kujikinga. Baadhi ya dalili za magonjwa ni joto kali la mwili, kudhoofu mwili, ngozi kusinyaa, kukohoa muda mrefu, kuharisha, kutapika na kukosa hamu ya kula.

**Vifaa/zana:** Picha mbalimbali, pichamguso, televisheni

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandaa orodha ya majina ya magonjwa mbalimbali yanayomwathiri binadamu;
ii) kutaja majina ya magonjwa hayo;
iii) kutaja dalili za ugonjwa aliowahi kuugua;
iv) kubaini dalili za magonjwa mbalimbali kwa kutumia picha mbalimbali au televisheni; na
v) kubaini hatua za kuchukua baada ya kuugua.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Je ugonjwa wa malaria una dalili zipi?

**Husisha**

Ukiwa nyumbani ulishawahi kuugua ugonjwa gani?

**Tumia**

i) Je, ni vifaa gani hutumika kijikinga na magonjwa?
ii) Taja dalili za ugonjwa wa kipindupindu.

**Shughuli ya 3.** Kuchambua njia za kujikinga na magonjwa mbalimbali

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kuimarisha stadi za kujimudu kwa kuchambua njia za kujikinga na magonjwa mbalimbali. Baadhi ya njia hizo ni kutumia chandarua, usafi wa mwili na mazingira, chanjo, kupima afya mara kwa mara, kuepuka ngono, kutoshirikiana vitu vyenye ncha kali.

**Vifaa/zana:** Picha mbalimbali, televisheni, matini mbalimbali, picha mguso, michoro au michoro mguso

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandaa orodha ya majina ya magonjwa mbalimbali yanayomwathiri binadamu;
ii) kutaja aina ya ugonjwa aliowahi kuugua;
iii) kutaja njia anazoweza kuzitumia kujikinga na magonjwa mbalimbali;
iv) kutaja hatua alizochukua kuepuka kuugua ugonjwa aliowahi kupata; na
v) kuzifafanua njia za kujikinga na magonjwa.

Ongoza majadiliano ya wanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira

**Tafakari**

Je, ni zipi njia za kujikinga na kipindupindu?

**Husisha**

Kwanini tunakunywa maji safi na salama?

**Tumia**

Unatumia chandarua kujikinga na ugonjwa gani?

# Sura ya kwanza

## Kusoma

### Utangulizi

Sura hii inahusu namna ya kumjengea umahiri wa kusoma mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Umahiri huu umegawanyika katika umahiri mahususi; kutambua sauti za herufi, kutambua uhusiano wa sauti na herufi, kusoma kwa ufasaha, na kusoma na kusikiliza kwa ufahamu. Kila umahiri mahususi umegawanyika katika shughuli ndogondogo za kutendwa na mwanafunzi ambapo mbinu mbalimbali zimependekezwa kutumika katika kufundishia na kujifunzia.

### Kutambua sauti za herufi

**Shughuli ya 1:** Kubaini sauti katika maneno

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kubaini sauti, umbo na alama za irabu.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadimguso za herufi na chati mguso.

### Hatua za kufuata

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubaini mawasiliano ya asili ya mwanafunzi;
ii) kuchunguza maumbo, sauti na alama mbalimbali za irabu a, e, i, o, u;
iii) kuonesha namna anavyoweza kubaini maumbo, sauti na alama mbalimbali za irabu a, e, i, o, u;
iv) kuumba maumbo na alama za irabu a, e, i, o, u na kutamka sauti za irabu hizo kwa kutumia michoro, picha, vifani, vitu halisi, tahajia ya vidole, Breille;
v) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya uumbaji wa maumbo na alama za irabu a, e, i, o, u na kutamka sauti za irabu hizo kwa kutumia michoro, picha, vifani, vitu halisi, tahajia ya vidole na Breille; na
vi) kutumia maarifa aliyoyapata katika shughuli mbalimbali akiwa ndani na nje ya darasa.

### Shughuli za ujifunzaji

Ongoza majadiliano na mawasiliano ya wanafunzi kwa mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Onesha picha /picha mguso/ alama/vifani na vitu halisi vya irabu a, e, i, o, u.

**Husisha**

Taja irabu na kuhusianisha na picha /picha mguso/ alama/vifani na vitu halisi vya irabu a, e, i, o, u.

**Tumia**

Tumia picha /picha mguso/ alama/vifani na vitu halisi kuumba irabu.

**Shughuli ya 2:** Kuunganisha sauti za irabu ili kuunda maneno

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuunganisha sauti za irabu ili kuunda maneno yatakayotumika kuendana na muktadha.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubaini irabu atakazotumia kuunda maneno mbalimbali kutokana na muktadha;
ii) kuunda maneno kwa kutumia irabu;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya uundaji wa maneno kwa kutumia irabu a, e, i, o, u; na
iv) kuunda maneno kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha matukio mbalimbali uliyokutana nayo katika mazingira unayoishi.

**Husisha**

Onesha tofauti ya matukio mbalimbali katika mazingira yako.

Tumia

i) Tumia vitu halisi, picha, kifani kumsaidia mwanafunzi kuunda maneno.
ii) Buni igizo/mchezo/shughuli fupi kuelezea matukio mbalimbali.

**Shughuli ya 3:** Kutambua sauti za konsonanti kwenye maneno

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kutambua sauti za konsonanti.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati mguso

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuchunguza maumbo, sauti na alama mbalimbali za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch) kwenye maneno;

ii) kubaini maumbo, sauti na alama mbalimbali za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch) kwenye maneno;

iii) kuumba maumbo na alama za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch) kwenye maneno kwa kutumia michoro, picha, vifani na vitu halisi;

iv) kutamka sauti za konsonanti kwa kutumia michoro, picha, vifani na vitu halisi;

v) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya uumbaji wa maumbo na alama za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch) kwenye maneno na kutamka sauti za konsonanti hizo kwa kutumia michoro, picha, vifani vitu halisi; na

vi) kutumia maarifa aliyoyapata katika shughuli mbalimbali akiwa ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mawasiliano ya wanafunzi kwa mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Onesha picha /picha mguso/ alama/vifani na vitu halisi vya konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch).

**Husisha**

Taja konsonanti na kuhusianisha na picha /picha mguso/ alama/vifani na vitu halisi vya konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch).

**Tumia**

Tumia picha /picha mguso/ alama/vifani na vitu halisi kuumba konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch).

**Shughuli ya 4:** Kutambua herufi kubwa na ndogo

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kutambua na kuumba herufi kubwa na ndogo.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi, chati mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubaini maumbo ya herufi kubwa na ndogo kwenye maandishi ya Braille na ya kimacho;
ii) kuunda maneno kwa kutumia herufi kubwa na ndogo kwenye maandishi ya Braille na ya kimacho;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya uundaji wa maumbo ya herufi kubwa na ndogo kwenye maandishi ya Braille na ya kimacho; na
iv) kuumba herufi kubwa na ndogo kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Taja maneno mbalimbali unayoyafahamu yenye herufi kubwa na ndogo.
ii) Je, utatumia alama gani kuandika herufi kubwa katika Breille?

**Husisha**

Onesha tofauti ya maneno yenye herufi kubwa na ndogo.

**Tumia**

Tumia vitu halisi, picha, kifani kumwezesha mwanafunzi kutambua herufi kubwa na ndogo.

**Shughuli ya 5:** Kuunganisha sauti za konsonanti na irabu ili kuunda silabi Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuunda silabi kwa kutumia muunganiko wa konsonanti na irabu.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati mgus

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuorodhesha irabu anazozifahamu;
ii) kuorodhesha konsonanti anazozifahamu;
iii) kuunganisha konsonanti na irabu kwa kutumia maumbo, picha, michoro, alama, vifani na vitu halisi kuunda silabi;
iv) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya uundaji wa silabi kwa kuunganisha konsonanti na irabu; na
v) kuunda silabi kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha silabi mbalimbali kwenye maneno.

**Husisha**

Tumia sauti za konsonanti na irabu kuunda silabi mbalimbali.

**Tumia**

Tumia vitu halisi, picha, kifani kuunda silabi mbalimbali.

**Shughuli ya 6:** Kutenganisha kwa kutamka sauti za konsonanti na irabu zilizounda silabi na silabi zilizounda maneno.

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kutenganisha kwa kutamka/ kuonesha sauti za konsonanti na irabu zilizounda silabi na silabi zilizounda maneno.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati mguso

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha silabi mbalimbali za maneno;
ii) kutumia silabi kuunda maneno mbalimbali;
iii) kuvunjavunja maneno ili kubaini silabi;
iv) kuvunjavunja silabi ili kubaini sauti za konsonanti na irabu;

v) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kutenganisha kwa kutamka/ kuonesha sauti za konsonanti na irabu zilizounda silabi na silabi zilizounda maneno; na
vi) kutenganisha sauti za konsonanti na irabu zilizounda silabi na silabi zilizounda maneno kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Bainisha majina ya vitu mbalimbali vinavyopatikana ndani na nje ya darasa.
ii) Onesha silabi mbalimbali zilizojenga majina ya vitu ulivyovibaini.

**Husisha**

Tofautisha silabi mbalimbali zinazojenga maneno kwa kutumia vitu halisi, picha na kifani.

**Tumia**

Tumia silabi mbalimbali kuunganisha maneno yenye maana katika miktadha mbalimbali.

**Shughuli ya 7:** Kutambua sauti za herufi mwambatano kwenye maneno

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kutambua sauti za herufi mwambatano kwenye maneno.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) Kubainisha maneno yaliyoundwa kwa herufi mwambatano;
ii) kuonesha herufi mwambatano kwenye maneno aliyoyabaini;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kutambua sauti za herufi mwambatano kwenye maneno; na
iv) kutambua sauti za herufi mwambatano kwenye maneno kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha majina ya wanafunzi yenye herufi mwambatano darasani/shuleni.

**Husisha**

Tofautisha maneno yaliyoundwa kwa herufi mwambatano na ambayo hayajaundwa kwa herufi mwambatano.

**Tumia**

Unda maneno mbalimbali kwa kutumia herufi mwambatano.

**Shughuli ya 8:** Kuunganisha sauti za herufi mwambatano na irabu ili kuunda silabi
Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuunganisha sauti za herufi mwambatano na irabu ili kuunda silabi.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuorodhesha sauti na maumbo yenye herufi mwambatano;
ii) kuorodhesha irabu;
iii) kuunganisha sauti zenye herufi mwambatano na irabu ili kuunda silabi zenye sifa ya herufi mwambatano;
iv) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kuunganisha sauti za herufi mwambatano na irabu ili kuunda silabi; na
v) kuunganisha sauti za herufi mwambatano na irabu ili kuunda silabi kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha majina ya wanafunzi yenye herufi mwambatano darasani na shuleni kwako.

**Husisha**

Tofautisha maneno yaliyoundwa kwa herufi mwambatano na ambayo hayajaundwa kwa herufi mwambatano.

**Tumia**

Unda maneno mbalimbali yenye herufi mwambatano.

Kutambua uhusiano wa sauti na herufi

**Shughuli ya 1:** Kuhusianisha sauti na herufi za irabu katika matini

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuhusianisha sauti na herufi za irabu katika matini.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuorodhesha herufi za irabu;
ii) kutamka sauti za irabu;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kuhusianisha sauti na herufi za irabu; na
iv) kuhusianisha sauti, umbo la Breille au tahajia ya vidole na herufi za irabu kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Tafuta maneno yenye sauti za irabu (a, e, i, o, u) yanayopatikana katika mazingira yako.
ii) Soma maneno hayo kwa sauti.

**Husisha**

Tofautisha utamkaji wa maneno yenye sauti za irabu (a, e, i, o, u).

Tofautisha uumbaji katika Breille na tahajia ya vidole na maneno yenye sauti za irabu (a, e, i, o, u)

**Tumia**

Tumia sauti za irabu (a, e, i, o, u) kutamka maneno mbalimbali.

**Shughuli ya 2:** Kuhusianisha sauti na herufi na konsonanti katika matini

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuhusianisha sauti na herufi za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch) katika matini.

**Vifaa/zana**:Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia,

kadi mguso za herufi na chati mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuorodhesha herufi za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch);
ii) kutamka sauti za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch);
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kuhusianisha sauti na herufi za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch); na
iv) kuhusianisha sauti na herufi za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch); kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Bainisha maneno yenye sauti za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch); yanayopatikana katika mazingira yako.
ii) Soma maneno uliyoyabainisha kwa sauti na kwa tahajia ya vidole.

**Husisha**

Tofautisha utamkaji wa maneno yenye sauti za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch).

**Tumia**

Tumia sauti za konsonanti (b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f, j); (g, y, z, h, r, w, v, ch); kutamka maneno mbalimbali.

**Shughuli ya 3:** Kuhusianisha sauti za herufi za konsonanti mwambatano katika matini

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuhusianisha sauti za herufi za konsonanti mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw) katika matini.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuorodhesha herufi za konsonanti mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw);
ii) kutamka sauti za konsonanti mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw);
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kuhusianisha sauti za herufi za konsonanti mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw); na
iv) kuhusianisha sauti na herufi za konsonanti mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw); kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.
v) Kutambua konsonanti mwambatano zinazosimama badala ya neno katika maandishi ya Breille (ch, sh, th, nd, ng, sw, dh).

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Bainisha maneno yenye sauti za konsonanti mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw); yanayopatikana katika mazingira yako.
ii) Soma maneno uliyoyabainisha kwa sauti.

**Husisha**

Tofautisha utamkaji wa maneno yenye sauti za konsonanti mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw).

**Tumia**

Tumia sauti za konsonanti mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw); kutamka maneno mbalimbali.

**Shughuli ya 4:** Kuunganisha sauti za herufi za konsonanti mwambatano na irabu ili kusoma silabi katika makundi yote.

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuunganisha sauti za herufi za konsonanti mwambatano (sh, th, mb, ny, ng, nd, kw, mw) na irabu ili kusoma silabi katika makundi yote.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha sauti na maumbo yenye herufi mwambatano;
ii) kuorodhesha irabu;
iii) kuunganisha sauti zenye herufi mwambatano na irabu ili kuunda silabi;
iv) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kuunganisha sauti za herufi za konsonanti mwambatano na irabu ili kusoma silabi; na
v) kuunganisha sauti za herufi za konsonanti mwambatano na irabu ili kusoma silabi kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Orodhesha majina ya wanafunzi yenye herufi mwambatano darasani/shuleni.

**Husisha**

Tofautisha maneno yaliyoundwa kwa herufi mwambatano na ambayo hayajaundwa kwa herufi mwambatano.

**Tumia**

Unda maneno mbalimbali yenye herufi mwambatano.

**Shughuli ya 5:** Kuunganisha silabi ili kusoma maneno

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuunganisha silabi ili kusoma maneno.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia,

kadi mguso za herufi na chati za maneno mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuorodhesha silabi kutoka kwenye maneno mbalimbali;
ii) kuunganisha silabi na silabi ili kusoma maneno;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kuunganisha silabi ili kusoma maneno; na

iv) kuunganisha silabi ili kusoma maneno kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Orodhesha majina ya wanafunzi darasani/shuleni kwa kuunganisha silabi mbalimbali.

**Husisha**

Tofautisha maneno yaliyoundwa kwa silabi zenye herufi mwambatano na zisizo na herufi mwambatano.

**Tumia**

Unda maneno mbalimbali kwa kutumia silabi.

**Shughuli ya 6:** Kutenganisha kwa kutamka sauti mojamoja ili kuunda maneno Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kutenganisha kwa kutamka sauti mojamoja ili kuunda maneno.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati za maneno mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuorodhesha maneno mbalimbali anayoyajua;

ii) kuorodhesha sauti za herufi za maneno aliyoyaorodhesha;

iii) kutenganisha sauti mojamoja za maneno aliyoyaorodhesha;

iv) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kutenganisha kwa kutamka sauti mojamoja ili kuunda maneno; na

**v)** kutenganisha kwa kutamka sauti mojamoja ili kuunda maneno kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Orodhesha maneno mbalimbali yenye maana kwa kuunganisha sauti.

**Husisha**

Tofautisha sauti za maneno uliyoyaorodhesha.

**Tumia**

Tenganisha sauti za maneno uliyoyaorodhesha kwa kutamka sauti mojamoja.

**Shughuli ya 7:** Kuunganisha maneno ili kusoma sentensi

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuunganisha maneno ili kusoma sentensi.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati za maneno mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

Kwa kutumia maandishi yaliyokuzwa, maandishi ya Breille, picha, alama, vifani, alama mguso na vitu halisi, mwongoze mwanafunzi.

i) kuorodhesha maneno mbalimbali anayoyafahamu;
ii) kuunganisha maneno mbalimbali ili kusoma sentensi;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kuunganisha maneno ili kusoma sentensi; na
iv) kuunganisha maneno ili kusoma sentensi kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Orodhesha maneno mbalimbali unayoyafahamu kutokana na mazingira yako.

**Husisha**

Tofautisha maneno ya watu, vitu, wanyama na miti.

**Tumia**

Unda sentensi mbalimbali kutokana na maneno uliyoyaorodhesha.

**Kusoma kwa ufasaha**

**Shughuli ya 1:** Kusoma kwa sauti kifungu cha habari/hadithi linganifu kwa kuzingatia matamshi sahihi ya maneno na uumbaji sahihi wa tahajia ya vidole na lugha ya alama ya mguso.

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kusoma kwa sauti kifungu cha habari/hadithi linganifu kwa kuzingatia matamshi sahihi ya maneno yaliyo katika mfumo

wa maandishi yaliyokuzwa, maandishi ya Breille, picha, alama, vifani, alama mguso na vitu halisi, mwongoze mwanafunzi.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia,

kadi mguso za herufi na chati za maneno mguso na video za lugha ya alama LAT.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha matini zenye habari mbalimbali;
ii) kusoma habari mbalimbali zilizomo katika matini;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kusoma kwa sauti kifungu cha habari/hadithi linganifu kwa kuzingatia matamshi sahihi ya maneno; na
iv) kusoma kwa sauti kifungu cha habari/hadithi linganifu kwa kuzingatia matamshi sahihi ya maneno kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Kusanya matini mbalimbali zenye habari zilizo katika mifumo nyumbufu.

**Husisha**

Tofautisha habari mbalimbali kutoka kwenye matini ulizozikusanya.

**Tumia**

Soma habari mbalimbali zilizopo kwenye matini kwa kuzingatia matamshi sahihi ya maneno.

**Shughuli ya 2:** Kusoma kwa sauti kifungu linganifu cha habari/hadithi kwa kasi stahiki (maneno 40 kwa dakika)

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kusoma kwa sauti kifungu linganifu cha habari/hadithi kwa kasi stahiki kulingana na mazingira halisi.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati za maneno mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha matini mbalimbali zenye habari mbalimbali;
ii) kusoma habari mbalimbali zilizomo katika matini mbalimbali kwa kasi stahiki kwa kuona na kuona, kugusa;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kusoma kwa sauti kifungu linganifu cha habari/hadithi kwa kasi stahiki, usahihi katika lugha ya alamamguso na Breill; na
iv) kusoma kwa sauti/ kugusa kifungu linganifu cha habari/hadithi kwa kasi stahiki kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Kusanya matini zenye habari mbalimbali katika mifumo nyumbufu.

**Husisha**

Tofautisha habari mbalimbali kutoka kwenye matini ulizozikusanya.

**Tumia**

Soma habari mbalimbali zilizopo kwenye matini kwa kasi stahiki.

**Shughuli ya 3:** Kusoma kwa sauti kifungu linganifu cha habari/hadithi kwa hisia na kwa kuzingatia alama za uandishi.

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kusoma kwa sauti kifungu linganifu cha habari/hadithi kwa hisia na kwa kuzingatia alama za uandishi zilizo katika mifumo nyumbufu.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati za maneno mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha matini zenye habari mbalimbali;
ii) kusoma habari mbalimbali zilizomo katika matini kwa hisia na kwa kuzingatia alama za uandishi (nukta, mkato, alama ya kuuliza na alama ya mshangao);

iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kusoma kwa sauti kifungu linganifu cha habari/hadithi kwa hisia na kwa kuzingatia alama za uandishi; na

iv) kusoma kwa sauti kifungu linganifu cha habari/hadithi kwa hisia na kwa kuzingatia alama za uandishi kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Kusanya matini zenye habari mbalimbali zilizo katika mifumo nyumbufu.

**Husisha**

Tofautisha habari kutoka kwenye matini ulizozikusanya.

**Tumia**

Soma habari zilizopo kwenye matini kwa hisia na kwa kuzingatia alama za uandishi (nukta, mkato, alama ya kuuliza na alama ya mshangao).

**Kusoma na kusikiliza kwa ufahamu**

Shughuli ya 1: Kutafsiri na kueleza picha

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kutafsiri na kueleza picha zilizo katika mfumo nyumbufu.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati za maneno mguso.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha picha zenye matukio mbalimbali;
ii) kutafsiri na kuelezea picha zenye matukio mbalimbali;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kutafsiri na kuelezea picha; na
iv) kutafsiri na kuelezea picha kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha picha zenye matukio mbalimbali zilizo katika mfumo nyumbufu.

**Husisha**

Tofautisha picha mbalimbali ulizozibainisha.

**Tumia**

Tafsiri picha mbalimbali zenye matukio mbalimbali.

**Shughuli ya 2:** Kubashiri maudhui ya habari/hadithi kwa usahihi kwa kutumia picha, jina la habari/hadithi na msamiati uliochaguliwa.

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kubashiri maudhui ya habari/hadithi kwa usahihi kwa kutumia picha, jina la habari/hadithi na msamiati uliochaguliwa kwa kuzingatia mfumo nyumbufu kulingana na mahitaji ya ujifunzaji.

**Vifaa/zana:** Matini za hadithi, chati za picha mguso, kadi sa sentensi, kibao fumbo, picha zinazozungumza, kibao cha kuandikia Braille na zana nyingine zinazopatikana katika mazingira.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha picha zenye matukio mbalimbali;
ii) kubashiri maudhui ya habari/hadithi kwa usahihi kwa kutumia picha;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kubashiri maudhui ya habari/ hadithi kwa usahihi kwa kutumia picha, jina la habari/hadithi na msamiati uliochaguliwa; na
iv) kubashiri maudhui ya habari/hadithi kwa usahihi kwa kutumia picha, jina la habari/hadithi na msamiati uliochaguliwa kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha picha zenye matukio mbalimbali.

**Husisha**

Tofautisha picha ulizozibainisha.

**Tumia**

Bashiri maudhui ya habari/hadithi kwa usahihi kwa kutumia picha, jina la habari/ hadithi na msamiati uliochaguliwa.

**Shughuli ya 3:** Kusikiliza habari/hadithi kwa ufahamu

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kusikiliza habari/hadithi kwa ufahamu kwa kutumia milango mbalimbali ya ufahamu kulingana na mahitaji yake.

**Vifaa/zana:** Vitetemezi na vitu halisi (mf. ngoma, redio, swichi mbalimbali)

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha habari/hadithi kutoka katika vyanzo mbalimbali;
ii) kusikiliza habari/hadithi kwa ufahamu;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo ya kusikiliza habari/hadithi kwa ufahamu; na
iv) kusikiliza habari/hadithi kwa ufahamu kwa kumpa mazoezi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha habari mbalimbali kutokana na mazingira yako.

**Husisha**

Tofautisha habari/hadithi mbalimbali ulizozibainisha.

**Tumia**

Simulia hadithi mojawapo uliyosimuliwa.

# Sura ya pili

## Kuandika

### Utangulizi

Sura hii inahusu kumjengea umahiri wa kuandika mwanafunzi mwenye uziwi kutoona. Umahiri huu umegawanyika katika umahiri mahususi; kumudu misingi ya kuandika, kumudu stadi za kuandika na kutumia kanuni za uandishi. Aidha kila umahiri mahususi umegawanyika katika shughuli ndogondogo ambazo zimefafanuliwa katika umahiri husika.

### **Shughuli ya 1.** Kutumia stadi za awali za kuandika

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuwa mahiri katika kutumia stadi za awali za kuandika kwa kuzingatia mfumo nyumbufu.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi, chati za maneno mguso na zana nyingine zinazopatikana kwenye mazingira husika.

### Hatua za kufuata

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandika hewani, vibao vya seli ya Breille (pre Braille);
ii) kuandika mchangani/cubarithm board;
iii) kuandika katika kibaoni/A4 frame au 2 line frame;
iv) kuandika kwenye daftari/karatasi ya Braille;
v) kuimarisha stadi ya kuandika kwa kurudiarudia ili kumudu misingi ya kuandika; na
vi) kumudu misingi ya kuandika kwa kumpa kazi mbalimbali ndani na nje ya darasa.

### Shughuli za ujifunzaji

Ongoza majadiliano ya wanfunzi kwa kutuma THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Chora michoro/maumbo yanayowakilisha irabu kwa kuzingatia mfumo nyumbufu.

**Husisha**

Tofautisha michoro mbalimbali inayoendana na irabu.

**Tumia**

Andika irabu ya kwanza na ya mwisho kwa kuzingatia hatua.

**Shughuli ya 2:** Kuchora michoro ya herufi.

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuwa mahiri katika kuchora

michoro ya herufi mbalimbali kwa kuzingatia mifumo nyumbufu.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, kibao na kitobozi, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi na chati za maneno mguso, machine ya kuchapia maandishi ya Breille, mchele, gundi, maharage, ulezi, msasa na zana nyingine zinazopatikana kwenye mazingira husika.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha herufi zenye kichwa;
ii) kubainisha herufi zenye pembe;
iii) kubainisha herufi zenye mkia;
iv) kubaini namba zinazounda herufi katika Breille;
v) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia ili kumudu kuchora michoro ya herufi; na
vi) kumudu kuchora michoro ya herufi kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Baini maumbo kwenye makundi yanayoonesha kichwa, pembe na mkia.

Husisha

i) Chora maumbo ya herufi inayokaribia kufanana.
ii) Taja herufi za Breille zinazokabiliana katika uandishi.

**Tumia**

i) Tumia namba za herufi za Breille kubaini herufi
ii) Tumia maumbo uliyoyachora kubaini herufi.

**Shughuli ya 3:** Kufuatisha herufi kwa kuzingatia hatua

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri wa kuumba herufi kwa hatua kwa kuzingatia mfumo nyumbufu.

**Vifaa/zana:** Vifani vya alfabeti, karatasi, kibao na kitobozi, michele, maharahe na vitu vingine vinavyopatikana kwenye mazingira.

**Hatua za kufuata**

Kwa kutumia mfumo nyumbufu, mwongoze mwanafunzi:

**i)** kuchora mzunguko wa kwanza/chora umbo la seli za juu za Braille **a** **e** **i** **o** **u**

**ii)** kuchora mzunguko wa pili/chora umbo la seli za chini za Braille **a** **e** **i** **o** **u**

**iii)** kuchora mzunguko wa tatu/fuatisha herufi kwa kuzingatia hatua. **a** **e** **i** **o** **u**

**iv)** kuchora mzunguko wa nne **a** **e** **i** **o** **u**

v) kufanya matendo ya kurudia rudia kwa kufuatisha herufi kwa kuzingatia hatua.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Bainisha herufi zenye hatua nne katika kuchora.
ii) Bainisha upande sahihi wa mkono unaoutumia kuunda herufi katika tahajia ya vidole.

**Husisha**

i) Tofautisha uumbaji wa tahajia ya vidole katika herufi na namba.
ii) Tofautisha hatua za uchoraji wa herufi mbalimbali.

**Tumia**

Tumia kanuni kuunda herufi

**Kumudu stadi za kuandika**

**Shughuli ya 1:** Kuandika herufi ndogo za irabu na konsonanti kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua.

Shughuli hii inalenga kujenga mwanafunzi kuwa mahiri katika kuandika herufi ndogo za irabu na konsonanti(b, m, k, d, n); (l, t, p, s, f. j); (g, y, z, h, r, w v, ch) kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi, chati za maneno mguso na zana nyingine zinazopatikana kwenye mazingira husika.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kundaa kadi / seli za Braille za herufi ndogo;
ii) kuhusianisha kadi/seli za herufi ndogo na maandishi ubaoni/hewani;
iii) kuandika herufi/seli za Breille za herufi ndogo kwenye karatasi;
iv) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia kuandika herufi ndogo za irabu na konsonanti kwa kuzingatia hatua; na
v) kuandika herufi ndogo za irabu na konsonanti kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha majina ya vitu vitano vinavyopatikana darasani.

**Husisha**

Orodhesha majina ya vitu vya darasani na ya vitu vya ofisini.

**Tumia**

Andika maneno matano kwa herufi ndogo.

**Shughuli ya 2:** Kuandika herufi kubwa za irabu na konsonanti kwa mpangilio na kufuata hatua.

Shughuli hii inalenga kumjenga mwanafunzi kuwa mahiri katika kuandika herufi kubwa za irabu na konsonanti (B, M, K, D, N); (L, T, P, S, F. J); (G, Y, Z, H, R, W, CH) kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi, chati za maneno mguso na zana nyingine zinazopatikana kwenye mazingira husika.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandaa kadi / seli za Braille za herufi kubwa;
ii) kuhusianisha kadi/seli za herufi kubwa na maandishi ubaoni/hewani;
iii) kuandika herufi/seli kubwa kwenye daftari;
iv) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia kuandika herufi kubwa za irabu na konsonanti kwa kuzingatia hatua; na
v) kuandika herufi kubwa za irabu na konsonanti kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha maneno matano yenye herufi kubwa kwenye chati ya maneno.

**Husisha**

Orodhesha majina ya vitu vya darasani na vitu vya ofisini kwa herufi kubwa.

**Tumia**

Andika maneno matano kwa herufi kubwa.

**Shughuli ya 3:** Kuandika herufi mwambatano

Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri katika stadi ya kuandika

herufi mwambatano kwa kuzingatia mfumo nyumbufu.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi, chati za maneno mguso na zana nyingine zinazopatikana kwenye mazingira husika.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandaa kadi/seli za herufi mwambatano;

ii) kuhusianisha kadi/seli za herufi mwambatano na zile za ubaoni na za kwenye matini za Braille; na
iii) kuandika herufi mwambatano kwenye daftari/karatasi ya Braille.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Orodhesha maneno matano yenye herufi mwambatano.

**Husisha**

Andika majina yenye herufi mwambatano na yasiyo na herufi mwambatano.

**Tumia**

Unda maneno kadiri uwezavyo yenye herufi mwambatano.

**Shughuli ya 4:** Kuandika silabi zinazotokana na herufi za konsonati na irabu Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kuandika silabi zinazotokana na herufi za konsonanti na irabu kwa kuzingatia mfumo nyumbufu.

**Vifaa/zana:**Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi, chati za maneno mguso na zana nyingine zinazopatikana kwenye mazingira husika.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandaa kadi za herufi/seli kwa mfunmo wa Braille za silabi zinazotokana na herufi za konsonanti na irabu;
ii) kuhusianisha kazi za herufi/seli kwa mfumo wa Braille za silabi na maandishi ya ubaoni;
iii) kuandika kwenye daftari/karatasi ya Braille silabi zinazotokana na herufi za konsonanti na irabu;
iv) kuimarisha stadi ya silabi zinazotokana na herufi za konsonanti na irabu kwa kurudia rudia kwa kuzingatia hatua; na
v) kuandika silabi zinazotokana na herufi za konsonanti na irabu katika daftari/ karatasi za Braille.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha majina yenye silabi zinazotokana na herufi za konsonati na irabu.

**Husisha**

Orodhesha majina ya wanafunzi wa kike na wanafunzi wa kiume yenye silabi zinazotokana na herufi za konsonanti na irabu.

**Tumia**

Unda maneno yenye silabi zinazotokana na herufi za konsonanti na irabu.

**Shughuli ya 5:** Kuandika silabi za herufi mwambatano

Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kuandika silabi zenye

herufi mwambatano kwa kuzingatia mahitaji ya ujifunzaji.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi, chati za maneno mguso na zana nyingine zinazopatikana kwenye mazingira husika.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandaa kadi za herufi/ seli za Braille za silabi za herufi mwambatano;
ii) kuhusianisha kadi za herufi/ seli za Braille za silabi mwambatano na zile za ubaoni;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia kuandika herufi mwambatano;
iv) kuandika silabi zenye herufi mwambatano katika daftari/karatasi ya Braille; na
v) kuandika silabi za herufi mwambatano kwa kumpa kazi za mara kwa mara ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha maneno yenye silabi za herufi mwambatano.

**Husisha**

Tofautisha maneno yenye herufi mwambatano na yasiyo na herufi mwambatano.

**Tumia**

Andika majina ya mimea nje ya darasa yenye herufi mwambatano.

**Shughuli ya 6:** Kuandika sentensi fupi

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuwa mahiri katika kuandika sentensi fupi kwa kuzingatia mahitaji ya ujifunzaji.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi, chati za maneno mguso na zana nyingine zinazopatikana kwenye mazingira husika.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandaa kadi za sentensi/ seli za Braille za sentensi fupi;
ii) kuhusianisha kadi za sentesi fupi/seli za Braille za sentensi fupi na zile za ubaoni;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia kuandika sentensi fupi;
iv) kuandika sentensi fupi katika daftari/karatasi ya Braille; na
v) kuandika sentensi fupi kwa kumpa kazi za mara kwa mara ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha sentensi fupi fupi kuhusu vyakula unavyovipenda kutoka kwenye chati ya vyakula.

**Husisha**

Husianisha masomo unayopenda na yale usiyoyapenda kwa kutumia sentensi fupifupi.

**Tumia**

Tumia sentensi fupi kujitambulisha.

**Kutumia kanuni za uandishi**

**Shughuli ya 1.** Kubaini alama za uandishi

Shughuli hii ina lenga kumjengea mwanfunzi umahiri wa kubaini alama za uandishi kwa kuandika habari fupi kwa kufuata alama za uandishi katika matini kwa kuzingatia mfumo nyumbufu.

**Vifaa/zana:** Kadi za alfabeti, kadi za silabi, karatasi, vibao, vifaa vya kuandikia, kadi mguso za herufi, chati za maneno mguso na zana nyingine zinazopatikana kwenye mazingira husika.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kusimulia tukio lililopita kwa ufupi;
ii) kuandika tukio hilo kwenye ubao/karatasi;
iii) kuweka alama za uandishi;
iv) kutunga sentensi kwa kuzingatia alama za uandishi;
v) kusoma sentensi alizotunga;
vi) kuandika sentensi fupi kwa kumpa kazi za mara kwa mara ndani na nje ya darasa; na
vii) kuandika habari kwa kuzingatia alama za uandishi.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Andika ratiba yako ya siku kuanzia asubuhi mpaka jioni. Tumia alama za uandishi.

**Husisha**

Tofautisha ratiba yako na ya wanafunzi wenzako.

**Tumia**

Andika Habari fupi kuhusu mchezo unaoupenda kwa kuzingatia alama za uandishi.

# Sura ya tatu

## Demonstrate mastery of basic English language skills

### Introduction

This chapter orients you on the best and most feasible ways of developing English language competencies to the Deafblind pupil. Thus, it consists mainly of two specific competencies: developing listening and speaking skills in different contexts and developing early literacy and numeracy skills. Every specific competence has related activities proposed as benchmarks of the teaching and learning process.

### Develop listening and speaking skills in different contexts

**Activity 1:** Use sounds found in the environment to form singular and plural names of objects

This activity intends to equip a pupil with competencies of using singular and plural forms to name objects found in the environment in adaptive formats.

**Teaching and learning aids:** English Alphabetuc Charts, real objects like stones, trees, picture charts, Braille alphabet charts, pictures, tactile pictures and tactile documents.

**Steps to follow**

Guide a pupil to:

i. identify sounds, codes, forms, and objects found in the environment;
ii. relate sounds to familiar objects;
iii. introduce oneself;
iv. say goodbye to other
v. use sounds, signs, forms, codes, and objects to form singular words;
vi. construct phrase and sentences in plural form;
vii. make simple stories using singular and plural forms of names of objects found in the environment;
viii. use different Braille codes and language forms to communicate singular and plural forms of noun objects;
ix. reinforce skills through repetition of actions learnt by the pupil to recognise singular and plural forms; and
x. use different Braille codes and language forms to construct singular and plural words in and outside the classroom.

**Learning activities**

Discuss with the pupil using the Reflect, Relate, Apply principle in responsive ways.

**Reflection**

Identify pictures, codes, and objects in singular and plural forms from the available charts.

**Relate**

Differentiate singular and plural objects, words, signs, or codes.

**Apply**

Use different objects found in the environment to form singular and plural.

**Activity 2:** Listen and respond to simple sentences

This activity aims to equip a pupil with skills to communicate using simple sentences in tactile signs, signs, Braille, blended, or spoken forms depending on their respective contexts.

**Teaching and learning aids:**

Alphabet Charts, real objects like stones, trees, picture charts, Braille alphabet charts and pictures

**Steps to follow**

Guide a pupil to:

i) demonstrate ways they use to communicate;
ii) express their feelings in simple sentences like stand up, go out, jump, sit down, and come here;
iii) identify parts of their body;
iv) respond to simple sentences in communication;
v) use common greetings;
vi) reinforce skills through repetition of actions learnt by the pupil to express and respond to simple sentences; and
vii) use different codes to express and respond to simple structures in and outside the classroom activities.

**Learning activities**

Discuss with the pupil using the Reflect, Relate, and adaptively apply the principle.

**Reflection**

What events were you involved in to form simple sentences?

**Relate**

i) Identify situations in which you can form simple expressions.
ii) Identify different forms of responding to simple structures.

**Apply**

Use different forms to express and respond to ideas according to context.

**Develop early literacy and numeracy skills**

**Activity 1:** Manipulate phonemes/sounds (delete, add and substitute) to form new words

This activity intends to equip pupil with competencies to manipulate morphemes/ sounds in their sign and Braille formats to form words and to communicate ideas in different contexts.

**Teaching aids**

Alphabet charts, real objects like stones, trees, picture charts, Braille alphabet charts and pictures.

**Teaching steps**

Guide a pupil to:

i) form sounds (a-z);
ii) identify words with similar sounds (alliteration)
iii) form blended sounds;
iv) identify different morphemes that can be manipulated in words
v) add a sound to a morpheme to form new words;
vi) delete a sound from a morpheme to form new words;
vii) substitute a sound in a morpheme to form new words;
viii) reinforce skills through repetitions of actions learnt by the pupil to delete, add, and substitute sounds in morpheme to form new words; and
ix) use different Braille codes and language forms to delete, add, and substitute sounds in a morpheme.

**Teaching activities**

Discuss with the pupil using the Reflect, Relate, Apply principle according to contexts.

**Reflection**

Identify contexts in which you deleted, added, or substituted sounds in a morpheme to form a new word.

**Relate**

Differentiate morphemes that were formed through deleting, adding, or substituting sounds.

**Apply**

Use different situations to delete, add, or substitute sounds of a morpheme to form new words.

**Activity 2:** Produce English sounds in written words

This activity aims to build writing skills to communicate ideas in different contexts. The activity will eventually enable the pupil to use written forms in communication.

**Teaching and learning aids:** English Alphabet Charts, real objects like stones, trees, picture charts, Braille alphabet charts and pictures.

**Steps to follow**

Guide a pupil to:

i) identify letters of names of familiar objects found in the environment;
ii) form letters in different forms;
iii) differentiate between small and capital letters;
iv) form blended letters/Braille codes;
v) list different words of objects found in the environment;
vi) produce correct sounds of consonants and vowels;
vii) reinforce skills through repetition of actions learnt by the pupil to form, write, and produce correct sounds of written words/Braille codes; and
viii) use different codes to produce the sounds of the English language in and outside the classroom.

**Teaching and learning activities**

Discuss with a pupil using the Reflect, Relate, Apply principle according to contexts.

**Reflection**

Identify situations in which you can use small letters, capital letters and blended letters/Braille codes.

**Relate**

Write words about persons and objects that are found in the environment.

**Apply**

Use English sounds/Braille codes to read written texts.

**Activity 3:** Read and write simple English words

This activity intends to equip a pupil with skills to read and write simple English words in different formats.

**Teaching and Learning aids:**

Alphabet charts, real objects like stones, trees, picture charts, Braille alphabet charts, A4 frame and stylus, Braille machines, Braille papers and pictures.

**Steps to follow**

Guide a pupil to:

i) identify simple words of familiar objects that are found in the environment (e.g. dog, bag, sun);
ii) associate names with sounds;
iii) write simple words in the English language and Braille formats;
iv) reinforce skills through repetition of actions learnt by the pupil to form, write, and produce correct sounds of written words/Braille codes; and
v) use different codes to produce the sounds of the English language in and outside the classroom.

**Learning activities**

Discuss with the pupil using the Reflect, Relate, Apply principle according to contexts.

**Reflect**

Identify events, people, or objects that are found in the environment.

**Relate**

Show the difference between pictures and real objects found in the environment.

**Apply**

Use pictures and real objects to form simple words in the English language.

**Activity 4:** Read words with two consonant clusters

This activity aims to equip a pupil with skills to read words with two clusters in adaptive formats.

**Teaching and learning aids:**

Alphabet charts, real objects like stones, trees, picture charts, Braille alphabet charts, story books, pictures and list of words with two clusters

**Stapes to follow**

Guide a pupil to:

i) identify letters that can be blended in a word;
ii) form words with two letters (e.g. bl, cl, dr, fr, fl, sn, st, sp, tw, sh, th);
iii) read words with two letters and sounds;
iv) reinforce skills through repetitions of action learnt by the pupil to form, write, and produce correct sounds of two letters in written/Braille codes; and
v) use different formats to produce the right sounds of the English language words with two letters in and outside the classroom.

**Teaching and learning activities**

Discuss with the pupil using the Reflect, Relate, Apply principle according to contexts.

**Reflect**

Identify events, people, or objects that are found in the environment.

**Relate**

Show the difference between pictures and real objects/ with two letters that are found in the environment.

**Apply**

Use pictures and real objects to form simple words with two letters in the English language.

**Activity 5:** Read and write simple sentences

This activity intends to equip a pupil with skills to read and write simple sentences in the English language using written or Braille codes.

Teaching and learning aids: Alphabet charts, real objects/names like stones, trees, picture charts, Braille alphabet charts, pictures, A4 frames and stylus and papers.

**Steps to follow**

Guide a pupil to:

i) identify pictures or real objects found in familiar in the environment;
ii) describe what pictures/real objects contain;
iii) write simple sentences about the pictures/real objects;
iv) reinforce skills through repetition of actions learnt by the pupil to form, write, and produce simple sentences in written/Braille codes; and
v) use different formats to produce simple sentences of the English language words in and outside the classroom.

**Teaching and learning activities**

Discuss with the pupil using the Reflect, Relate, Apply principle according to contexts.

**Reflect**

Identify events, people, or objects that are found in the environment.

**Relate**

Differentiate between pictures and real objects with two letters that are found in the environment.

**Apply**

Use pictures and real objects to form simple sentences in the English language.

**Activity 6:** Use basic punctuation marks in sentences

This activity aims to enable a pupil to acquire skills in using punctuation marks in producing English language sentences in adaptive formats.

Teaching and learning aids: Alphabet charts, real objects like stones, trees, picture charts, Braille alphabet charts, pictures, A4 frames and stylus and papers

**Steps to follow**

Guide a pupil to:

i) identify punctuation marks (comma, full stop, question mark);
ii) use commas in simple sentences in the English language;

iii) use a full stop in simple English language sentences;
iv) use a question mark in interrogating sentence;
v) reinforce skills through repetition of actions learnt by the pupil to use commas, full stops, and question marks to produce simple sentences in written/Braille codes; and
vi) use different formats to produce simple sentences of the English language words in and outside the classroom using punctuation marks.

**Learning activities**

Discussion with the pupil using the Reflect, Relate, Apply principle according to contexts.

**Reflection**

Give an expression that you may use to ask your friend to give you some water.

**Relate**

Demonstrate situations in which you may use punction marks to form simple structures.

**Apply**

Use pictures and real objects to form simple words using punctuation marks in the English language.

**Activity 7:** Express days of the week and months of the year

This activity intends to equip pupil with competencies in expressing days of the week and months of the year.

**Teaching and learning aids:**

Alphabet charts, real objects (e.g. stones, radio, trees) picture charts, Braille alphabet charts, pictures, A4 frames and stylus, papers and calendar charts.

**Steps to follow**

Guide a pupil to:

i) identify days of the week from the chart;
ii) differentiate months of the year from a calendar;
iii) reinforce skills through repetition of actions learnt by the pupil to use calendars to mention days of the week and months of the year; and
iv) use different formats to differentiate days of the week and months of the year in and outside the classroom.

**Learning activities**

Discuss with the pupil using the Reflect, Relate, Apply principle according to contexts.

**Reflection**

i) Identify the days of the week you go to school.
ii) Identify the month you were born.

**Relate**

What are months of your school holiday?

**Apply**

Use pictures and real objects to tell days and months.

# Sura ya Nne

## Kuhesabu

### Utangulizi

Sura hii inahusu kumjengea umahiri wa kuhesabu mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Umahiri huu umegawanyika katika umahiri mahususi; kutambua dhana ya namba, kutumia matendo ya kihisabati na kutumia dhana za kihisabati. Kila umahiri mahususi umegawanyika katika shughuli ndogondogo za kutendwa na mwanafunzi ambapo vifaa/zana mbalimbali zimependekezwa kutumika katika kufundishia na kujifunzia shughuli husika.

### Kutambua dhana ya namba

**Shughuli ya 1:** Kubaini dhana ya namba kwa kutumia vitu katika mazingira Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri wa kubaini dhana ya namba kwa kutumia mazingira yanayomzunguuka ili kuzitumia katika shughuli za kihisabati. Stadi hizi zitajengwa kumwezesha mwanafunzi kujenga uwezo wa kutumia mazingira yake.

**Vifaa/zana:** Picha za kuchorwa zenye rangi, picha mguso, vifani, vitu halisi na matini mbalimbali.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubaini dhana ya namba kwa kutumia picha/pichamguso;
ii) kubaini vitu vilivyomo darasani mwake;
iii) kuhesabu kila kitu alichokibaini ili kujua idadi yake;
iv) kuandika idadi ya kila kitu alichokibaini ndani ya darasa lake;
v) kuelezea wanafunzi wenzake idadi ya kila kitu alichokibaini darasani mwake;
vi) kutaja aina za namba kwa kutumia picha, vifani na matini mbalimbali zenye unamu tofautitofauti; na
vii) kutaja sifa za namba kwa kutumia picha na chati inayoonesha namba.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira kwa kuzingatia mifumo nyumbufu.

**Tafakari**

Je, umejifunza nini kuhusu dhana ya namba?

**Husisha**

Kuna vitu vingapi vilivyomo darasani?

**Tumia**

Andika idadi ya kila kitu ulichokibaini ndani ya darasa lako.

**Shughuli ya 2:** Kubaini namba kuanzia 1-999 kwa tarakimu na maneno

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kujenga stadi za kubaini namba kuanzia 1-999 kwa tarakimu na maneno atakazoweza kuzitumia katika maisha yake ya kila siku wakati na baada ya shule. Aidha, stadi hizi zitajengwa kwa njia ya kumshirikisha mwanafunzi katika kubaini namba kuanzia 1-999 kwa tarakimu na maneno.

**Vifaa/zana**

Picha mguso, picha za kuchorwa zenye rangi na unamu mbalimbali, abakasi, sinia la namba, cubarithm board na matini mbalimbali.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kutumia vihesabio/sinia la namba/ abakasi ili kubaini namba kuanzia 1-999 kwa tarakimu na maneno kwa kutumia maandishi ya Braille na ya kimacho;
ii) kutenganisha mamoja, makumi kisha mamia kwenye kihesabio chake, sinia la namba au abakasi na cuberithm board;
iii) kuandika namba kwenye karatasi;
iv) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia namba kwa kuzingatia hatua; na
v) kuandika namba kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza zoezi la mwanafunzi Kubaini namba kuanzia 1-999 kwa tarakimu na maneno kwa kuona au kupapasa.

**Tafakari**

i) Bainisha idadi ya mamoja katika kumi.
ii) Bainisha idadi ya makumi inayopatikana katika mia moja.

**Husisha**

Tofautisha idadi ya mamoja kwenye kumi na idadi ya makumi kwenye mia moja.

**Tumia**

Andika namba ulizobaini kuanzia 1-999 kwa tarakimu na maneno.

**Shughuli ya 3.** Kupanga namba kwa mfuatano 1-999

Shughuli hii inalenga kumuwezesha mwanafunzi kujenga stadi za kupanga namba kwa mfuatano 1-999 kulingana na hatua za ujifunzaji.

**Vifaa/zana:**Picha, pichamguso, michoro, michoromguso, abakasi, sinia la namba, “cubarithm board”

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kutumia vihesabio/sinia la namba/ abakasi/ “cubarithm board” ili Kupanga namba kwa mfuatano kuanzia 1-999 kwa kutumia maandishi ya Braille na ya kimacho;
ii) kupanga namba kwa kuzingatia mfuatano wa mamoja, makumi kisha mamia kwenye kihesabio chake, sinia la namba, “cubarithm board” au abakasi;
iii) kuandika kwenye karatasi kwa kufuata mpangilio wa mamoja, makumi na mamia;
iv) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia namba kwa kuzingatia hatua; na
v) kuandika namba kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza wanafunzi kupanga namba kwa mfuatano kuanzia 1-999 kwenye daftari au karatasi ya Braille.

**Tafakari**

Eleza mpangilio wa namba kwa kuzingatia mtiririko wa 1-999.

**Husisha**

Rekebisha mpangilio wa namba uliopewa kwa kuzingatia mpangilio wa namba 1-999.

**Tumia**

Cheza mchezo wa kuhesabu namba kwa kufuata mpangilio wa 1-999.

**Kutumia matendo ya kihisabati**

**Shughuli ya 1.** Kutambua namba katika makumi na mamoja

Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kutambua namba katika makumi na Mamoja.

**Vifaa/zana:** Vifani, Picha, pichamguso, michoro, michoromguso, abakasi, sinia la namba na "cubarithm board"

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kutumia vihesabio/sinia la namba/ abakasi/ "cubarithm board" kutambua namba katika mamoja na makumi;
ii) kupanga namba kwa kuzingatia mfuatanao wa mamoja, makumi kisha mamia kwenye kihesabio chake, sinia la namba, cubarithm board au abakasi;
iii) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia namba kwa kuzingatia hatua; na
iv) kuandika namba kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza wanafunzi kutambua namba katika mamoja na makumi kwenye kitabu au karatasi ya Braille.

**Tafakari**

Je, umejifunza nini kuhusu kutambua namba katika mamoja na makumi?

**Husisha**

Rekebisha makundi ya namba yaliyopangwa bila kufuata mpangilio na kuweka kwenye makundi sahihi.

**Tumia**

Wanafunzi wacheze mchezo wa kutambua namba kutoka kwenye kadi za namba za kimacho na Braille.

**Shughuli ya 2.** Kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kujumlisha

Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kujumlisha.

**Vifaa/zana:** Vitu halisi, vifani, picha, pichamguso, michoro, michoromguso, abakasi, sinia la namba, "cubarithm board" na kompyuta

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kutumia vihesabio/sinia la namba/abakasi/ cubarithm board/kikokotozi kumudu dhana ya kujumlisha;

ii) kupanga namba kwa kuzingatia mfuatano wa mamoja, makumi kisha mamia kwenye kihesabio chake, sinia la namba, cubarithm board au abakasi ili aweze kumudu dhana ya kujumlisha;

iii) kupitia hesabu mbalimbali za kujumlisha ili kujenga dhana ya kujumlisha;

iv) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia namba kwa kuzingatia hatua; na

v) kuandika namba kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza wanafunzi kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kujumlisha.

**Tafakari**

Bainisha mazoezi ya kutambua dhana ya kujumlisha.

**Husisha**

Husianisha hesabu mbalimbali ili kujenga dhana ya kujumlisha.

**Tumia**

Tumia michezo mbalimbali kutambua dhana ya kujumlisha

**Shughuli ya 3:** Kujumlisha namba kupata jumla isiyozidi 999

Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kujumlisha namba kupata jumla isiyozidi 999.

**Vifaa/zana:** Vitu halisi, Vifani, Picha, picha mguso, michoro, michoro mguso, abakasi, sinia la namba na cubarithm board.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kutumia vihesabio/sinia la namba/ "*acubarithm board*"/kikokotozi katika kujumlisha namba kupata jumla isiyozidi 999;

ii) kujumlisha namba kupata jumla isiyozidi 999 kwenye kihesabio chake, sinia la namba, cubarithm board au abakasi;

iii) kujumlisha namba kupata jumla isiyozidi 999;

iv) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia namba kwa kuzingatia hatua; na

v) kuandika namba kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza wanafunzi kujumlisha namba mbalimbali na kupata jumla isiyozidi 999.

**Tafakari**

Bainisha michezo kujumlisha namba mbalimbali na kupata jumla isiyozidi 999.

**Husisha**

Husianisha hesabu mbalimbali ili kujenga dhana ya kujumlisha jumla isiyozidi 999.

**Tumia**

Tumia maumbo yaliyopo kupata jumla isiyozidi 999.

**Shughuli ya 4:** Kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kutoa

Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kutoa.

**Vifaa/zana:** Vitu halisi, vifani, picha, pichamguso, michoro, michoro mguso, abakasi, sinia la namba na “cubarithm board”

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kutumia vihesabio/sinia la namba/ abakasi/ “cubarithm board”/kikokotozi katika kutoa namba zisizozidi 999;
ii) kutoa namba zisiyozidi 999 kwenye kihesabio chake, sinia la namba, “cubarithm board” au abakasi;
iii) kutoa namba na kupata jibu la lisilozidi 999;
iv) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia namba kwa kuzingatia hatua; na
v) kuandika namba kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza wanafunzi kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kutoa.

**Tafakari**

Bainisha michezo kutoa namba mbalimbali.

**Husisha**

Husianisha hesabu mbalimbali ili kujenga dhana ya kutoa.

**Tumia**

Tumia maumbo yaliyopo kutoa namba mbalimbali.

**Shughuli ya 5:** Kutoa namba zisizozidi 999

Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kutoa namba zisizozidi 999.

**Vifaa/zana:** Vitu halisi, vifani, picha, pichamguso, michoro, michoromguso, abakasi, sinia la namba na "cubarithm board"

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kutumia vihesabio/sinia la namba/ abakasi/ "cubarithm board"/kikokotozi katika kutoa namba zisizozidi 999;

ii) kutoa namba zisiyozidi 999 kwenye kihesabio chake, sinia la namba, "cubarithm board" au abakasi;

iii) kutoa namba na kupata jibu la lisilozidi 999;

iv) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia namba kwa kuzingatia hatua; na

v) kuandika namba kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza wanafunzi kutoa namba mbalimbali na kupata majibu yenye namba isiyozidi 999.

**Tafakari**

Baini namba mbalimbali kupata jumla isiyozidi 999.

**Husisha**

Wanafunzi kupitia na kuhakiki hesabu mbalimbali za kutoa na kupata jumla isiyozidi 999.

**Tumia**

Tumia namba zilizopo kupata jumla isiyozidi 999.

**Kutumia dhana za kihisabati**

**Shughuli ya 1:** Kubaini maumbo ya msingi

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kujenga umahiri wa kubaini dhana ya maumbo ya msingi kwa kutumia mazingira yanayomzunguka.

**Vifaa/zana:** Vitu halisi, vifani, picha, pichamguso, michoro, michoromguso, abakasi, sinia la namba na "cubarithm board", na "spur wheel" na "rubber mat"

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubaini maumbo ya msingi yaliyomo darasani;

ii) kuunda maumbo ya msingi;

iii) kupitia maumbo ya msingi kwenye matini mbalimbali;

iv) kutofautisha aina mbalimbali za maumbo ya msingi katika mazingira yake ndani na nje ya darasa;

v) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia namba kwa kuzingatia hatua; na

vi) kuandika namba kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza zoezi la wanafunzi kuzunguuka darasa huku wakibain maumbo mbalimbali kwa kuona au kugusa.

**Tafakari**

Bainisha umbo la darasa letu.

**Husisha**

Tofautisha umbo la darasa letu na lile la bustani yetu.

**Tumia**

Tumia maumbo mbalimbali kubaini umbo la darasa.

**Kutumia matendo ya kihisabati**

**Shughuli ya 1:** Kutumia vitu/ TEHAMA kumudu dhana ya kuzidisha kama kujumlisha makundi yanayolingana

Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kuzidisha kama kujumlisha makundi yanayolingana.

**Vifaa/zana:** Vitu halisi, vifani, picha, picha mguso, michoro, michoro mguso, abakasi, sinia la namba, cubarithm boards, kompyuta, na kibao cha Braille.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kutumia vihesabio/sinia la namba/ abakasi/ "*cubarithm board*"/kikokotozi kumudu dhana ya kuzidisha kama kujumlisha makundi yanayolingana;

ii) kuzidisha namba kwa kuzingatia mfuatanao kwenye kihesabio chake, sinia la namba, cubarithm board au abakasi ili aweze kumudu dhana ya kuzidisha kama kujumlisha makundi yanayolingana;

iii) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia namba kwa kuzingatia hatua; na

iv) kuandika namba kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza wanafunzi kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kuzidisha kama kujumlisha makundi yanayolingana.

**Tafakari**

Bainisha maumbo mbalimbali ya kuzidisha kama kujumlisha makundi yanayolingana.

**Husisha**

Tumia hesabu mbalimbali ili kujenga dhana ya kuzidisha kama kujumlisha makundi yanayolingana.

**Tumia**

Tumia namba mbalimbali ili kujenga dhana ya kuzidisha kama kujumlisha makundi yanayolingana.

**Shughuli ya 2:** Kuzidisha namba kwa tarakimu moja kupata zao lisilozidi 999 Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kuzidisha namba kwa tarakimu moja kupata zao lisilozidi 999.

**Vifaa/zana:** Vitu halisi, vifani, picha, pichamguso, michoro, michoromguso, abakasi, sinia la namba, "cubarithm boards", kompyuta, na kibao cha Braille

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kutumia vihesabio/ abakasi/ "cubarithm board"/kikokotozi kumudu dhana ya kuzidisha namba kwa tarakimu moja kupata zao lisilozidi 999;

ii) kuzidisha namba kwa kuzingatia mfuatano kwenye kihesabio chake, cubarithm board au abakasi ili aweze kumudu dhana ya kuzidisha namba kwa tarakimu moja kupata zao lisilozidi 999;

iii) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia namba kwa kuzingatia hatua; na

iv) kuandika namba kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Waongoze wanafunzi kuzidisha ili kujenga dhana ya kuzidisha namba kwa tarakimu moja kupata zao lisilozidi 999.

**Tafakari**

Zidisha namba kwa tarakimu moja kupata zao lisilozidi 999.

**Husisha**

Bainisha hesabu mbalimbali zilizozidishwa kwa tarakimu moja ili kujenga dhana ya kuzidisha namba kwa tarakimu moja kupata zao lisilozidi 999.

**Tumia**

Tumia namba moja ili kujenga dhana ya kuzidisha namba kwa tarakimu moja kupata zao lisilozidi 999.

**Shughuli ya 3**: Kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kugawanya kama kutoa makundi yanayolingana. Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kugawanya kama kutoa makundi yanayolingana.

**Vifaa/zana:** Vitu halisi, Vifani, Picha, pichamguso, michoro, michoromguso, abakasi, sinia la namba, “cubarithm boards”, kompyuta, na kibao cha Braille.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha namba zinazoweza kugawanyika;

ii) kutumia vihesabio/ abakasi/ cubarithm board/kikokotozi kutumia vitu/ TEHAMA kumudu dhana ya kugawanya;

iii) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia namba kwa kuzingatia hatua; na

iv) kugawanya namba kwa mpangilio kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza wanafunzi kutumia Kutumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kugawanya kama kutoa makundi yanayolingana.

**Tafakari**

Bainisha vitu vinavyoweza kugawanywa kwa kutumia vitu/TEHAMA.

**Husisha**

Tofautisha namba zinazoweza kugawanyika na zisizoweza kugawanyika kwa kutumia vitu/TEHAMA.

**Tumia**

Tumia vitu/TEHAMA kumudu dhana ya kugawanya kama kutoa makundi yanayolingana.

**Kutumia dhana za kihisabati**

**Shughuli ya 1:** Kubaini dhana ya sehemu kwa kutumia vitu halisi na TEHAMA (nzima, nusu, robo, theluthi, theluthi mbili).

Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kubaini dhana ya sehemu kwa kutumia vitu halisi na TEHAMA (nzima, nusu, robo, theluthi, theluthi mbili).

**Vifaa/zana:** Vitu halisi, Vifani, Picha, picha mguso, michoro, michoro mguso, abakasi, sinia la namba, cubarithm boards, kompyuta, na kibao cha Braille.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubaini maumbo mbalimbali ya sehemu (nzima, nusu, robo, theluthi, theluthi mbili) kwa kutumia vitu halisi na TEHAMA;

ii) kutofautisha aina za maumbo katika mazingira;

iii) kuimarisha stadi kwa kurudia rudia namba kwa kuzingatia hatua; na

iv) kuchora maumbo mbalimbali kwa kutumia vitu/TEHAMA kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza wanafunzi kubaini dhana ya sehemu kwa kutumia vitu halisi na TEHAMA (nzima, nusu, robo, theluthi, theluthi mbili).

**Tafakari**

Bainisha maumbo kwa kutumia vitu/TEHAMA ili kubaini dhana ya sehemu (nzima, nusu, robo, theluthi, theluthi mbili).

**Husisha**

Tofautisha aina ya maumbo uliyoyabainisha.

**Tumia**

Tumia vitu/TEHAMA kuchora maumbo mbalimbali (mf. nzima, nusu, robo, theluthi, theluthi mbili).

**Shughuli ya 2:** Kutumia stadi za vipimo katika miktadha mbalimbali

Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kutumia stadi za vipimo katika miktadha mbalimbali.

**Vifaa/zana:** Vitu halisi, vifani, picha, picha mguso, michoro, michoro mguso, abakasi, sinia la namba, "cubarithm boards", kompyuta, na kibao cha Braille.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kupima maumbo katika miktadha mbalimbali;

ii) kupima maumbo ya msingi yaliyomo darasani;

iii) kuumba maumbo katika miktadha mbalimbali;

iv) kutofautisha aina mbalimbali za maumbo katika mazingira ya ndani na nje ya darasa; na

v) Kuimarisha stadi kwa kujirudia rudia vipimo kwa kuzingatia hatua kwa kumpa kazi za ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza mwanafunzi kupima maumbo ili kutumia stadi za vipimo katika miktadha mbalimbali.

**Tafakar**i

Chambua maumbo unayoweza kuyatumia kwenye michezo.

**Husisha**

Tofautisha maumbo uliyoyachambua.

**Tumia**

Tumia maumbo uliyoyachambua kuandaa michezo mbalimbali.

# Sura ya Tano

## Kuthamini Utamaduni, Sanaa na Michezo

### Utangulizi

Sura hii inahusu namna ya kumjengea umahiri wa kuthamini utamaduni, sanaa na michezo mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Umahiri huu umegawanyika katika umahiri mahususi; kuthamini utamaduni wake na wa watu wengine, kuheshimu tofauti za kiimani, kuonesha matendo ya kimaadili, kubuni kazi za sanaa, na kushiriki katika michezo mbalimbali. Kila umahiri mahususi umegawanyika katika shughuli ndogondogo za kutendwa na mwanafunzi.

### Kutathimini wake na wa watu wengine

**Shughuli ya 1.** Kubaini vyakula vya Kitanzania

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuwa mahiri katika kubaini vyakula vya kitanzania.

**Vifaa/zana:** Kadi na chati za picha za video zinazohusu utamaduni, sanaa, michezo ya asili na michoromguso zinazoonesha vyakula vya kitanzania.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuchunguza michoro na picha zinazoonesha aina za vyakula mbalimbali;

ii) kugusa na kupapasa aina mbalimbali za vyakula;

iii) kufanya ziara ya kutembelea stoo au duka la shule kubaini aina mbalimbali za vyakula; na

iv) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia kwa kushiriki shughuli za kijamii ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ufundishaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Ni vyakula gani ulivyovibaini dukani au kwenye stoo ya shule?

**Husisha**

Je ni vyakula gani ambavyo vipo dukani vinafanana na unavyokula shuleni?

**Tumia**

Ni vyakula gani unakula kila siku shuleni ?

**Shughuli ya 2:** Kubaini mavazi ya kitanzania

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kubaini mavazi ya kitanzania ili kumjengea mtazamo chanya juu ya asili ya Kitanzania.

**Vifaa/zana:** Picha mguso/ mchoromguso unaoonesha aina mbalimbali za mavazi ya kitanzania, picha za tamaduni na vitu halisi

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuchunguza michoro na pichamguso zinazooonesha aina mbalimbali ya mavazi;
ii) kuchunguza mavazi mbalimbali ya Kitanzania;
iii) kueleza tofauti za mavazi hayo kwa kugusa au kupapasa; na
iv) kufanya matendo ya kuvaa mavazi.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Ni mavazi gani uliyowahi kuvaa?

**Husisha**

Eleza tofauti kati ya mavazi mabaya na mazuri.

**Tumia**

Ni mavazi gani unayavaa shuleni na nyumbani?

**Shughuli ya 3.** Kubaini makazi ya asili ya Kitanzania

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kubaini makazi ya asili ya Kitanzania ili kuheshimu utamaduni wa wake na wa watu wengine.

**Vifaa/zana:** pichamguso/ michoromguso inayoonesha aina mbalimbali za makazi ya asili ya Kitanzania.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuchunguza michoro na picha mguso zinazoonesha aina mbalimbali ya makazi ya asili ya kitanzania;

ii) kuchunguza makazi ya asili ya Kitanzania;

iii) kueleza tofauti za makazi ya asili;

iv) kuchora mavazi ya asili; na

v) kufanya ziara ya mafunzo kutembelea maeneo ya karibu yenye nyumba za kiasili.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Ni makazi gani ya asili yaliyo katika mazingira unayoishi?

**Husisha**

i) Makazi hayo yanafafana na makazi uliyojifunza darasani?

ii) Je, nyumba yenu inafanana na nyumba ulizojifunza darasani?

**Tumia**

Je, makazi ya asili yanatumika kufanya nini ?

**Shughuli ya 3.** Kucheza ngoma na kuimba

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuwa mahiri katika kucheza ngoma, kuimba, na kufanya shughuli mbalimbali za kijamii.

**Vifaa/zana:** Sanaa na michezo iliyorekodiwa, vifilimbi, ngoma na pichamguso/

michoro mguso inayoonesha watu wakicheza ngoma.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuchunguza michoro na picha mguso inayoonesha watu wakicheza ngoma;

ii) kuchunguza vifaa vya kuchezea ngoma kama vile; filimbi, ngoma;

iii) kuimba wimbo anaufahamu; na

iv) kuimba wimbo na kucheza ngoma hatua kwa hatua.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira .

**Tafakari**

Ulipocheza ngoma na kuimba ulijisikiaje?

**Husisha**

i) Shuleni kwenu mnacheza ngoma gani?

ii) Je, mnacheza ngoma hiyo wakati gani?

**Tumia**

Ni vifaa gani unavyotumia katika kucheza ngoma?

**Kuheshimu tofauti za kiimani**

**Shughuli ya 1**. Kueleza imani za watu wanaotuzunguka

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuwa mahiri katika kuelezea imani za watu wanaomzunguka.

**Vifaa/zana:** Sauti zilizorekodiwa watu wakiwa katika maeneo ya kuabudu, vifani mbalimbali vinavyotumika mahali pa kuabudia na pichamiguso za nyumba za ibada.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuchunguza michoro na pichamguso au vifani vinavyotumika katika nyumba za ibada;

ii) kutembelea sehemu ya karibu kwenye nyumba za ibada kulingana na imani yake; na

iii) kutaja vitu na mambo aliyojifunza katika ziara yake.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Ulipotembelea sehemu za ibada ulibaini nini?

**Husisha**

i) Ni sehemu gani watu hufanya ibada?

ii) Je, watu huenda kwenye nyumba za ibada siku gani?

**Tumia**

Ni vitu gani vinatumika katika ibada?

**Shughuli ya 2:** Kuhusianisha imani na maadili mema

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuhusianisha imani na maadili mema kwa kuzingatia tamaduni za kitanzania.

**Vifaa/zana:** Michoro/ picha zinazoonesha matendo ya maadili

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuchunguza michoro na pichamguso zinazoonesha maadili mema;

ii) kufanya matendo yanayoonesha imani na maadili mema anayoyatenda kila siku; na

iii) kuonesha matendo ya imani ya watu wengine.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Ni maadili gani unayoyaonesha kila siku?

**Husisha**

i) Maadili hayo yanafanyika wakati gani?

ii) Ni matendo gani ya imani watu wanayoyafanya kila siku?

**Tumia**

Je matendo gani yanatumika kila siku watu wanapokwenda kwenye nyumba za kuabudu?

**Kumbuka:** Mwalimu kumbuka kuzingatia imani ya kila mwanafunzi wakati wa ufundishaji wa umahiri huu.

**Shughuli ya 3.** Kushiriki katika shughuli za kijamii

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kubaini shughuli mbalimbali za jamii za Kitanzania ambazo anaweza kushiriki kulingana na muktadha.

**Vifaa/zana**: Michoro/picha zinazoonesha shughuli mbalimbali za kijamii

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuchunguza michoro na pichamguso inayoonesha shughuli za kijamii;

ii) kutembelea maeneo ya shuleni kwake mfano dukani, sehemu zinazouza chakula kuchunguza shughuki hizo; na

iii) kufanya ziara katika maeneo ya karibu nje ya shule kubaini shughuli za kijamii.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Ni shughuli gani ulizibaini zinazofanyika shuleni kwako?

ii) Ni shughuli gani ulizozibaini nje ya shule?

**Husisha**

Ni shughuli gani za kijamii ulizozibaini nje ya shule unazozifanya kila siku?

**Tumia**

Ni shughuli gani za kijamii unazifanya kila siku shuleni na nyumbani?

**Kuonesha matendo yenye maadili**

**Shughuli ya 1**. Kutenda matendo yenye maadili

Shughuli hii inalenga kumjengenea mwanafunzi umahiri wa kutambua na kutenda matendo yenye maadili katika jamii ya kitanzania.

**Vifaa/zana:** Michoro/ picha zinazoonesha matendo ya maadili.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha matendo yenye maadili na yasiyo na maadili;

ii) kutambua shughuli yenye maadili;

iii) kubabaini umuhimu wa shughuli zenye maadili;

iv) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo yenye maadili; na

v) kutumia matendo yenye maadili ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Bainisha matendo yasio na maadili uliyoyafanya.

ii) Eleza kwanini matendo hayo hayana maadili.

**Husisha**

Tofautisha matendo yenye maadili na yasiyo na maadili shuleni na nyumbani.

**Tumia**

Tumia picha na michoro kuonesha matendo mbalimbali yenye maadili na yasiyo na maadili.

**Shughuli ya 2:** Kutenda matendo yanayoonesha thamani ya watu wengine Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa kutambua matendo yanayothamini watu wengine katika jamii ya kitanzania.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha matendo yenye maadili na yasiyo na maadili;

ii) kutambua matendo yanayothamini watu wengine;

iii) kubabaini umuhimu wa matendo yanayothamini watu wengine;

iv) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia matendo yasiyo na maadili; na

v) kutumia matendo yenye kuthamini watu wengine ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha matendo yasiyothamini watu wengine.

**Husisha**

Tofautisha matendo yenye maadili na yasiyothamini watu wengine shuleni na nyumbani.

**Tumia**

Tumia picha na michoro kuonesha matendo mbalimbali yenye maadili na yanayothamini watu wengine.

**Kubuni kazi za sanaa**

**Shughuli ya 1.** Kushiriki katika sanaa za utendaji wa mikono (kufuma, kufinyanga, kuchonga, kushona, kupiga chapa, kutia nakshi)

Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa uundaji wa sanaa kwa kushiriki katika shunguli mbalimbali za mikono.

**Vifaa/zana:** Michoro/picha zinazoonesha sanaa na vitu halisi (mfano, maleba, njuga, shanga)

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha shughuli mbalimbali za sanaa;

ii) kushiriki katika sanaa mbalimbali za kufuma, kufinyanga, kuchonga, kuchora, kufinyanga;

iii) kubaini umuhimu wa shughuli shughuli za sanaa;

iv) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia utendaji wa mikono; na

v) kutengeneza sanaa mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha kazi mbalimbali za sanaa ulizowahi kuzifanya.

**Husisha**

Eleza namna ya kutumia mazingira kutengeneza sanaa mbalimbali.

**Tumia**

Tumia mazingira halisi kuunda sanaa mbalimbali.

**Shughuli ya 2.** Kushiriki katika sanaa za ubunifu wa sauti (ngojera, majigambo, vichekesho)

Shughuli hii inalenga kumjengea mwanafunzi umahiri wa ubunifu wa sanaa za sauti kwa kuzingatia utamaduni wa Kitanzania.

**Vifaa/zana:** Michoro/picha zinazoonesha sanaa, vitu halisi(mf. marimba, kayamba, ngoma, filimbi)

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha sanaa za sauti;

ii) kutengeneza makundi ya sanaa za sauti;

iii) kushiriki katika sanaa za sauti;

iv) kubaini umuhimu wa shughuli za sanaa;

v) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia sanaa za sauti; na

vi) kutengeneza sanaa mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha sanaa mbalimbali ulizokwisha fanya.

**Husisha**

Eleza namna ya kutumia mazingira kutengeneza sanaa tofautitofauti.

**Tumia**

Tumia mazingira halishi kuunda sanaa tofautitofauti.

**Shughuli ya 3.** Kushiriki katika sanaa za utendaji wa mwili (kuigiza, minjogeo ya mwili)

Shughuli hii inalenga kumjengeneza mwanafunzi umahiri wa uundaji wa sanaa kwa kutumia mwili kwa kuzingatia utamaduni wa Kitanzania.

**Vifaa/zana:** Michoro/picha zinazoonesha sanaa na vitu halisi.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuainisha shughuli za sanaa zinazotumia mwili;

ii) kushiriki katika sanaa za kuigiza na mijongeo ya mwili;

iii) kubaini umuhimu wa shughuli za sanaa;

iv) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia utendaji wa mwili; na

v) kutengeneza sanaa mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha kazi za sanaa ulizokwisha fanya.

**Husisha**

Eleza namna ya kutumia mazingira kutengeneza sanaa mbalimbali zinazohusisha utendaji wa mwili.

**Tumia**

Tumia mazingira halisi kuunda sanaa tofautitofauti.

**Kushiriki katika michezo mbalimbali**

Shughuli. Kucheza michezo sahili

Shughuli hii inalenga kumjengenea mwanafunzi umahiri wa kucheza michezo sahili kulingana na mazingira mbalimbali.

**Vifaa/zana:** Michoro/picha zinazoonesha michezo mbalimbali, vitu halisi(mfano, mpira, kamba na ngoma)

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubainisha michezo mbalimbali;

ii) kushiriki katika michezo;

iii) kubaini umuhimu wa michezo mbalimbali;

iv) kuimarisha stadi kwa kurudiarudia michezo mbalimbali; na

v) kucheza michezo mbalimbali ndani na nje ya darasa.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Bainisha michezo mbalimbali uliyokwisha cheza.

**Husisha**

Eleza namna ya kutumia mazingira ili kufanya michezo mbalimbali.

**Tumia**

Tumia mazingira halisi kubuni michezo mbalimbali.

# Sura ya Sita

## Kutunza afya na mazingira

### Utangulizi

Sura hii inahusu namna ya kumjengea umahiri wa kutunza afya na mazingira mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Umahiri huu umegawanyika katika umahiri mahususi; kutunza afya yake na jamii inayomzunguka, kujilinda na mazingira hatarishi, na kuchunguza vitu vilivyomo katika mazingira na kuwa na mtazamo chanya kuhusu mazingira. Kila umahiri mahususi umegawanyika katika shughuli ndogondogo ambazo zimefafanuliwa katika umahiri unaohusika.

**Shughuli ya 1:** Kusafisha mwili wake

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuwa mahiri katika kusafisha mwili wake.

**Vifaa/zana:** Chati za picha za nguo, Mayer Johnson symbols, vifaa halisi vya kusafishia mwili, na chati za pichamguso zinazohusu usafi wa mwili.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubaini sehemu za nje za mwili wake;
ii) kuchunguza pichamguso zinazoonesha sehemu ya mwili wa binadamu;
iii) kuimba wimbo unaohusu mwili wa binadamu;
iv) kueleza kazi za sehemu za nje za mwili wa binadamu;
v) kuchora mwili wa binadamu;
vi) kufanya usafi wa mwili wake hatua kwa hatua; na
vii) kufanya kazi za kujirudiarudia ili kumarisha stadi.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Umegusa nini katika mwili wako?
ii) Umegusa sehemu zipi za mwili wako?

**Husisha**

Je, ni sehemu gani zinazokuwezesha kuandika kazi za darasani?

**Tumia**

Ni sehemu gani za mwili wako unazozitumia kunusa na kugusa vitu?

**Shughuli ya 2.** Kutunza mavazi

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuwa mahiri katika kutunza mavazi yake.

**Vifaa/zana:** Chati za picha zinazohusu namna ya kutunza mavazi

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuchunguza pichamguso zinazohusu sehemu za kutunzia mavazi;

ii) kuchunguza vitu halisi vya kutunzia mavazi kama vile; kabati, shelfu, sanduku, begi; na

iii) kufanya matendo ya kutunza mavazi yake.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Ni wakati gani unafua nguo zako za shule?

ii) Baada ya kufua nguo zako za shule huziweka wapi?

**Husisha**

Ni vifaa gani huvitumia katika kutunza nguo zako?

**Tumia**

Ni vifaa gani unavyoweza kuvitumia kutunza mavazi yako?

**Kujilinda na mazingira hatarishi**

**Shughuli ya 1.** Kuepuka mazingira hatarishi

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kujilinda na mazingira hatarishi.

**Vifaa/zana:** Pichamguso za wanyama na pichamguso zinazoonesha maeneo hatarishi.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandaa chatimguso inayoonesha mazingira hatarishi, pichamguso za wanyama, pichamguso zinazoonesha maeneo hatarishi;

ii) kugusa pichamguso zilizoandaliwa ili wabaini mazingira hatarishi;

iii) kuonesha mazingira hatarishi kwa kugusa pichamguso na alama mguzo;

iv) kufanya matendo ya kuigiza kwa kutumia picha na matendo zinazohusu mazingira hatarishi;

v) kuchukua tahadhari ya maeneo hatarishi na namna ya kuepeuka; na

vi) kubuni michezo mbalimbali inayoonesha matendo hatarishi na kuonesha namna ya kuepuka matendo hayo.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Maeneo gani ya shule yana mazingira hatarishi?

ii) Umewezaje kutambua maeneo hatarishi?

**Husisha**

i) Je, umewahi kujikuta katika mazingira hatarishi?

ii) Je, ulipata tatizo lolote?

**Tumia**

i) Utamsaidiaje mwenzako aliyepata ajali katika maeneo hatarishi?

ii) Huwa unatumia viungo gani vya mwili kutambua eneo hatarishi?

**Shughuli ya 2.** Kubaini alama za usalama barabarani na katika mazingira Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuwa mahiri katika kutumia alama za usalama barabarani na katika mazingira yake.

**Vifaa/zana:** Alama za barabarani zilizorekodiwa kutokana na mazingira na alama mguso za usalama barabarani.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuandaa igizo dhima linalohusu namna ya kuzingatia alama za barabarani;

ii) kuigiza igizo hilo hatua kwa hatua;

iii) kubainisha matumizi ya alama za barabarani kwa kutumia alamamguso za usalama barabarani;

iv) kuelezea namna anavyozitumia alama hizo;

v) kufanya ziara katika mazingira yake ili kubaini alama za usalama barabarani; na

vi) kubuni michezo mbalimbali namna ya kutumia alama za barabarani kwa kuzingatia alama walizojifunza.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

i) Umejifunza nini kutokana na mchezo uliocheza?

ii) Matumizi sahihi ya alama za usalama barabarani yana faida gani?

**Husisha**

i) Ni kwa namna gani huwa unazitambua alama za barabarani kwenye mazingira?
ii) Ni alama gani za kwenye mazingira yako unazizingatia unapokuwa nje ya darasa?

**Tumia**

Fanya matembezi katika mazingira ya ndani na nje ya darasa ili kubaini alama zilizopo.

**Shughuli ya 3.** Kuzingatia alama za usalama barabarani katika mazingira Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuwa mahiri katika kuzingatia alama za barabarani katika mazingira anayoishi.

**Vifaa/zana:** Picha mguso na vitu halisi na mazingira hatarishi yaliyorekodiwa.

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kubaini alama mbalimbali za barabarani kwa kumgusisha pichamguso au alamamguso za alama za barabarani;
ii) kubaini alama za barabarani anazozitumia katika mazingira yake;
iii) kuigiza matendo ya kuzingatia alama za barabarani katika mzingira yake; na
iv) kufanya matendo ya kuzingatia alama za barabarani na za mazingira yake.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira.

**Tafakari**

Ni sehemu zipi katika mazingira yako kuna alama za usalama barabarani?

**Husisha**

Ni alama zipi umkutana nazo ulipoenda ofisi za walimu, chooni, darasani au mahali unapolala?

**Tumia**

i) Wakati gani unaweza kutumia alama ulizokutana nazo katika mazingira yako ?
ii) Ni alama gani ulizitumia wakati wa kuvuka barabara?

**Kuchunguza vitu vilivyopo katika mazingira**

**Shughuli ya 1.** Kufanya uchunguzi sahili wa viumbe hai na visivyo hai katika mazingira yanayotuzunguka.

Shughuli hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kuwa mahiri katika kufanya uchunguzi sahili wa viumbe hai na visivyo hai katika mazingira.

**Vifaa/zana:** Picha na michoro ya viumbe hai na visivyohai

**Hatua za kufuata**

Mwongoze mwanafunzi:

i) kuchunguza pichamguso na michoromguso viumbe vilivyo hai na visivo hai;
ii) kubainisha viumbe hai na visivyo hai kwa kutumia pichamguso au mchoro mguso;

iii) kuchunguza viumbe hai na visivyo hai katika mazingira yake; na

iv) kuandaa na kuigiza igizo hilo.

**Shughuli za ujifunzaji**

Ongoza majadiliano na mwanafunzi kwa kutumia THT kulingana na mazingira

**Tafakari**

Umejifunza nini kuhusu viumbe hai na visivyo hai?

**Husisha**

Tofautisha viumbe hai na visivyo hai.

**Tumia**

Unawezaje kuwatunza viumbe hai?

## Viambatanisho

Kabla ya kuandaa mpango binafsi wa kielimu wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona, ni muhimu mwalimu kuanza na uchunguzi/upimaji wa mwanafunzi. Zoezi hili ni muhimu ili kubaini aina na hali ya ulemavu, uwezo alionao mwanafunzi na utendaji wa milango baki ya fahamu katika ujifunzaji. Hii ni pamoja na kufahamu aina ya mawasiliano anayotumia na namna anavyoweza kujifunza. Kuathiriwa kwa uwezo wa kusikia na kuona kunasababisha hali ya uziwikutoona inayompa mwanafunzi changamoto za kushindwa kumudu ujifunzaji na hata kuyatumia mazingira yake kwa kuwasiliana na jamii inayomzunguka. Kuathirika kwa milango ya fahamu kunamfanya mwanafunzi mwenye uziwikutoona kushindwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa urahisi na pengine hata kushindwa kupata maana ya vitu vinavyomzunguka. Ili mwanafunzi aweze kumudu ujifunzaji na kuyatumia mazingira yake ni muhimu ajengewe stadi za kutumia milango yake ya fahamu. Matokeo ya uchunguzi ndiyo yatakayoongoza uandaaji wa mpango binafsi wa kielimu wa mwanafunzi, uchaguzi wa mbinu na zana za kufundishia na kujifunzia zitatumika kulingana na uwezo wa kila mwanafunzi kwa kuzingatia mahitaji maalumu aliyonayo.

Mpango binafsi wa kielimu wa mwanafunzi utakuwa ni dira ya kumsaidia mwalimu katika kuendana na mtiririko wa mambo ya msingi ya kuyafundisha kwa kuzingatia malengo makuu na malengo mahususi yaliyopangwa kwa pamoja na wazazi na watoa huduma wengine, ili kufikiwa kwa lengo la kumjengea mwanafunzi mwenye uziwikutoona stadi za maisha ya kujitegemea na kuzitumia awapo shuleni, nyumbani na katika jamii baada ya maisha ya shule.

### Mawasiliano na uhusiano wa kijamii

Mwalimu, chunguza jinsi mwanafunzi;

i) Anavyotoa sauti, ishara, alama, matumizi ya macho, mabadiliko ya mijongeo ya mwili na jinsi anavyotumia mdomo kutamka.
ii) Anavyopokea au kutoa taarifa.
iii) Anavyoitikia au anavyofuata maelekezo anayopewa.

Mijongeo ya misuli (hali ya utendaji wa misuli midogo na mikubwa)

i) Mwanafunzi anapenda au hapendi kufanya nini?
ii) Uvumilivu alionao akipewa kazi.
iii) Fikra tunduizi na mwitiko wake. (hali ya kutaka kujua jambo).
iv) Uwezo wa misuli katika utendaji wa jambo analopewa kulifanya.

v) Uwezo wa kunyoosha mikono, miguu na hata kujaribu kukifuata kitu alichopewa mbele yake.

vi) Uwezo wa kushika vitu.

vii) Ni kwa namna gani anasaidiwa, vitu gani vinatumika kumsaidia (kama vifaa saidizi) ili kumudu mijongeo?

viii) Kifaa/vifaa saidizi alivyonavyo vinamsaidia kwa kiwango gani?

ix) Ni mkao upi unaonekana kufaa kwake ili kumudu utendaji wa jambo lililo mbele yake?

x) Eneo lipi linaloonekana kufaa kwake ili kumudu utendaji wa jambo lililo mbele yake?

xi) Nini mwitiko wa hali ya mguso wa ngozi akigusa kitu/vitu tofautitofauti?

**Hali ya uoni**

Mwalimu umchunguze mwanafunzi kama ana baki ya uoni kwa kuzingatia yafuatayo:

i) Ni nini anapenda kukikazia macho zaidi?

ii) Ni wapi anapenda kukazia macho zaidi?

iii) Ni jinsi gani anatumia baki ya uoni wake kwa karibu (ukaribu kiasi gani)?

iv) Ni namna gani anatumia baki ya uoni wake kwa kuona mbali. (umbali gani)?

v) Hali ya uoni wa kati au pembeni?

vi) Je, anaonekana kuwa makini kutazama kitu kilichowekwa mbele ya macho yake au anaangalia pembeni?

vii) Ni rangi ipi au zipi anazoonesha kupenda zaidi?

viii) Je, kuna mapendekezo yoyote ya kutumia vifaa saidizi vya kukuza uoni kutoka kwenye taarifa zilizopita?

**Hali ya usikivu**

Mwalimu umchunguze mwanafunzi kama ana baki ya usikivu kwa kuzingatia kama:

i) Anabaini sauti zozote.

ii) Anaweza kufuatisha upande sauti iliko/inakotokea.

iii) Kuna sauti anazozipenda au kuzichukia.

iv) Anaitikia maelekezo wakati wa upimaji.

v) Kuna mapendekezo yoyote ya kutumia kifaa saidizi kutoka kwenye taarifa zilizopita.

**Kumbuka:** Mwalimu, unapaswa uandae utaratibu wa kumchunguza kila mwanafunzi masikio na macho yake mara kwa mara ili kubaini kama usikivu au uoni wake uko sawa, unapungua au unaongezeka. Aidha, ni muhimu pia kubaini milango bora ya ujifunzaji anayoonesha kuimudu mwanafunzi mfano; ya kuona, kusikia, kunusa, kugusa au kuonja.

## Kutumia baki ya usikivu (masikio)

Kiwango baki cha usikivu kinaweza kutumiwa na mwanafunzi mwenye uziwikutoona kwa kupokea sauti kutoka kwa mtu anayezungumza naye. Mwalimu, tumia kiwango baki cha usikivu wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona kwa kutoa sauti kubwa au kumpatia shimesikio itakayowezesha kukuza kiwango chake cha usikivu kulingana na mapendekezo ya mtaalamu wa audiolojia.

## Kutumia baki ya uoni (macho)

Kiwango baki cha uoni kinaweza kutumiwa na mwanafunzi mwenye uziwikutoona kwa kuona watu au vitu katika mazingira. Mwalimu, tumia kiwango baki cha uoni wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona kwa kukuza maandishi au picha, picha mguso na michoro, michoro mguso katika ujifunzaji na mawasiliano, kuyakoleza au kupaka rangi yenye kung'aa vyema ili mwanafunzi mwenye uziwikutoona aweze kutumia katika ujifunzaji. Aidha, mshirikishe mtaalamu wa macho ili apendekeze jinsi ya kutumia vifaa vya kumsaidia kukuza maandishi au kuongeza mwanga.

**Kutumia mlango baki wa kuonja (ulimi)**

Mlango wa kuonja unahusu uwezo wa kubaini ladha mbalimbali za vyakula kama vile; tamu, chachu, chungu na kali.

i) Mwalimu, unapaswa kumwezesha mwanafunzi kujijengea stadi za kutumia mlango wa kuonja. Hii itamwezesha kutambua ladha ya vitu kama; chumvi, sukari, ndimu au vinywaji.

ii) Mwalimu, unapaswa kuleta darasani vitu halisi mwelekeze mwanafunzi kufahamu majina na ladha ya vitu hivyo.

iii) Stadi ya kutumia mlango wa vionjo itamwezesha mwanafunzi kutumia viungo vya chakula kwa usahihi kwa mfano, kwenye mboga ataweka chumvi na kwenye chai ataweka sukari.

## Kutumia mlango baki wa kunusa (pua)

Mlango wa kunusa unahusu uwezo wa kubaini harufu kwa kutumia pua:

i) Mwanafunzi anapaswa kukuziwa stadi za kunusa ili aweze kutambua harufu za vitu vinavyofaa au visivyofaa kuliwa. Stadi hii itamsaidia pia kutambua mavazi yake na watu walioko katika mazingira yake.

ii) Mwalimu, unapaswa kuleta vitu halisi darasani. Mpatie mwanafunzi fursa ya kuvinusa. Vilevile awezeshwe kufahamu majina ya kila kilichonuswa.

Kumbuka: Mwalimu usilete darasani vitu hatarishi kama vile; pilipili iliyosagwa, sumu na tindikali na kumpa mwanafunzi kuvigusa au kuvinusa.

## Kutumia mlango baki wa kugusa na kupapasa (ngozi)

Mlango huu unahusu uwezo wa kubaini unamu wa vitu mbalimbali kwa kuvigusa au kuvipapasa. Mwalimu unapaswa kumwezesha mwanafunzi kujenga stadi hii ili aweze kuainisha vitu na watu walioko katika mazingira aliyopo kwa kugusa. Mwalimu unapaswa kuleta darasani vitu vyenye unamu tofauti vya kufundishia, kutambua kwa kugusa na kupapasa vitu hivyo vilivyo vigumu, laini, na vimiminika. Mfano ni kama unga wa mahindi na unga wa ngano, mchele, maharage na nguo zenye unamu mbalimbali. Vyote hivi ni vitendo muhimu sana katika kujenga dhana na matumizi yake katika maisha ya kila siku ya mwanadamu.

## Uandaaji wa azimio la kazi na andalio la somo

Ujifunzaji na ufundishaji ni tendo la uhusiano baina yako mwalimu na mwanafunzi. Ili tendo lifanyike ipasavyo, unapaswa kufanya maandalizi sahihi na ya kina kwa kuzingatia dira/lengo kusudiwa la stadi mahususi inayotarajiwa kujengwa na kutumiwa na mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Ni wajibu wa mwalimu katika kupanga au kufanya marekebisho ya nini kianze kufundishwa, nini kifuatie, kifundishwe kwa muda gani na katika mazingira yapi ya ujifunzaji. Hii itampasa mwalimu kufanya marekebisho ya azimio ili liwe rekebifu kwa kuandaa andalio la somo na mpango binafsi kulingana na mahitaji maalumu ya mwanafunzi.

Kabla ya kuandaa azimio, zingatia mambo ya msingi ikiwamo; uwezo wa kufikiri wa mwanafunzi wako, uwezo wa kuwasiliana, uwezo wa kunyumbulisha misuli mikubwa na midogo, uzoefu wake katika eneo linalohusika na mengine muhimu. Mwalimu chukua eneo la umahiri mkuu wa somo unaopatikana katika muhtasari ili kuhakikisha unachokusudia kukifundisha hakipishani na mtaala. Hivyo baada ya kujua umahiri mkuu uliobainishwa kwenye mtaala, andaa umahiri mahususi na shughuli ya kutendwa na mwanafunzi.

Mfano: Katika jedwali shughuli ya kutendwa na mwanafunzi iliyochaguliwa kwa mfano, kuumba maumbo mbalimbali. Wakati wa kufundisha/kufanya shughuli ya kuumba maumbo mbalimbali kuna umahiri wa kuhusianisha maumbo, kupanga aina za maumbo, kuweka maumbo katika makundi, kufuata mtiririko, kuweka katika utaratibu unaotakiwa. Pia, mjongeo wa misuli mikubwa na misuli midogo na kusaidia kazi kivikundi.

Sambamba na shughuli tajwa, mwalimu utamwezesha mwanafunzi mwenye uziwikutoona kujenga stadi za sanaa na michezo, afya na mazingira, matendo ya hisabati, mawasiliano, fikiratunduizi, uhusiano na nyingine nyingi zitakazoweza kumjengea mwanafunzi stadi mbalimbali atakazozikuza katika maisha yake ya kila siku.

Mwalimu utatakiwa kuwa mbunifu zaidi katika kutafuta shughuli itakayoweza kugusa nyanja zote za ujifunzaji wa mwanafunzi mwenye uziwikutoona. Hii ni kwasababu mwanafunzi mwenye uziwikutoona hushindwa kuwa makini katika ujifunzaji kwa kukaa sehemu moja tu kwa muda mrefu. Hivyo, mwalimu, katika ufundishaji zingatia mtiririko wa matukio yasipishane kati ya siku moja na siku zinazofuata hata kama wafundishaji watabadilika lakini mtiririko wa ufundishaji unatakiwa kubaki palepale ili kumzoesha mwanafunzi na kumfanya aelewe kwa urahisi. Wanafunzi wenye uziwikutoona ukivuruga utaratibu huchukua muda mrefu sana kuelewa dhana ndogo.